SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Mwanafunzi** wa miaka 11 alivyoozeshwa na bibi yake kwa mahari ya nguruwe

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Oktoba 18, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580737
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Rais Samia: Nitawaondoa wasiowajibika

**AWATAKA** wananchi kuwasema viongozi wasiotatua changamoto...

*Endelea ukurasa. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akimsalimia mtoto Samia Yona aliyezaliwa usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Jiji la Arusha muda mfupi baada ya kuizindua rasmi, Chekereni Arumeru mkoani Arusha. Aliyemshikilia mtoto huyo ni mama yake, Mary Joseph (34) mkazi wa Njiro. Rais Samia yupo mkoani Arusha kwenye ziara ya kikazi kutembelea, kukagua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ya wananchi. **PICHA: IKULU**



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo (katikati), akimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Shay-akye TRD, Shakiru Yahya, pasi ya kusafiria pamoja na tiketi ikiwa ni ishara ya kuwatakia safari njema kundi la wafan-yabiashara zaidi ya 100 wanaotarajiwa kwenda nchini Uturuki kushiriki Kongamano la Afrika la Uchumi na Biashara 2021, hafla hiyo imefanyika jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati wa Benki ya CRDB, Boma Raballa (kushoto), na Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa benki hiyo, Toyi Ruvumbagu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## HESLB yatoa bil. 99.9/- za mikopo awamu ya kwanza

UKURASA 2



## Serikali yaipatia SUMA JKT shamba la bil. 152/-

UKURASA 3

MICHEZO **MAYELE AIONYA KMC KWA YANGA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kesi nyingine ya Sabaya kunguruma wiki nzima

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KESI ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, leo itaanza kunguruma katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha kwa wiki nzima mfululizo.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanakabiliwa na mashtaka matano.

Hadi sasa mashahidi wa tatu wa Jamhuri katika shauri hilo, wameshapanda kizimbani kutoa ushahidi wao wa msingi mahakamani humo.

Shtaka la kwanza, kwenye kesi hiyo ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi Kifungu cha 57 (1) na 60 (2) na linawakabili washtakiwa wote.

Shtaka la pili, ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, na ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Kifungu cha 15 (1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la tatu, ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, linamkabili mshakiwa wa kwanza peke yake, kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15 (1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la nne, ni la matumizi mabaya ya madaraka, linalomkabili Sabaya peke yake, kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la tano, la utakatishaji wa fedha na linawakabili washtakiwa wote saba, ni kinyume na kifungu 12 (D),13 (1A), cha Sheria ya Utakatishaji Fedha sura ya 423 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

# Samia: Nitawaondoa wasiowajibika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewapa jeuri wananchi wa Mkoa wa Arusha, akiwataka kuwasema viongozi wasiowajibika na kuwafichua ili wabadilishwe.

Amewataka wananchi kuwataja hasa wateule wake ambao hawafanyi kazi za wananchi ikiwamo kutatua changamoto zao zinazowakabili.

Rais Samia aliwapa kazi hiyo wananchi jana, alipokuwa katika eneo la UsaRiver, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

"Endapo kiongozi anasimamia sheria hapo sawa, lakini kama hafuati sheria wananchi waseme ili abadilishiwe aletwe kiongozi mwingine," alisema.

Akizungumzia changamoto ya wafanyabiashara wa Soko la Tengeru, Rais Samia, alisema serikali italishughulikia kupitia Halmashauri ya Meru ili wafanyabiashara wauze bidhaa zao eneo soko la Tengeru na soko la zamani.

Kuhusu barabara ya Usa River-Mbuguni hadi Mirerani kilomita 29, alisema wanalishughulikia na kuwasihi wananchi kudumisha amani ili maendeleo yaweze kupatikana sambamba na miradi kujengwa katika kila wilaya na mikoa yote.

Akiwa eneo la Tengeru, Rais Samia alisema Tengeru wana changamoto kubwa ya barabara na kutoa rai kwa halmashauri kuweka vipaumbele katika barabara ili kuhakikisha barabara zinazotoa huduma za chakula zinawekewa changarawe ili zipitike.

Kuhusu tatizo la madai ya mafao ya malimbikizo ya mishahara katika mashamba ya maua, alisema, watalifanyia kazi na kuhusu soko la Tengeru, alisema soko hilo ni kubwa na linahudumia watu wengi, lakini hali hairidhishi.

"Naiagiza halmashauri kupitia kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru, Mwalimu Zainabu Makwinya, Mkuu wa Wilaya, Mhandisi Richard Ruyango na Mbunge John Pallangyo mkae kwa pamoja ili kuboresha soko hili ili siku nikija nikute soko lipo katika hali nzuri," alisema.

"Kaeni kitako ili soko hili liboreshwe, soko hili linabeba watu wengi, hivyo liboreshwe, liendane na hadhi ya ukubwa wa watu wengi."

Diwani wa Kata ya Akheri, Julius Mungure, aliomba mashine ya X-Ray ya digitali kwa sababu hawana japo waliiomba mashine hiyo kutoka Hospitali ya Mount Meru na kwamba changamoto kubwa waliyonayo soko la Karoti, Tengeru na Soko la Ndizi ni barabara ya lami au changarawe kwa sababu wafanyabiashara wanataabika na changamoto za masoko hayo.

Huku Mbunge wa Arumeru Mashariki, John Pallangyo, aliomba barabara ya Mbuguni kwenda Mirerani iangaliwe kwa kiwango cha lami.

Akiwa Kikatiti awali, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alimshukuru Rais Samia kwa kuleta miradi mbalimbali ya kimaendeleo ikiwamo uboreshaji wa sekta ya afya, maji na pia kiwanda cha nyama cha Longido kitafungua fursa za kiuchumi kwa wilaya hiyo, mkoa na kuingiza serikali mapato.o



Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA-JKT), Brigedia Jenerali Absolomon Shausi, wakikagua shughuli za kilimo zinazoendelea katika shamba la Mngeta wakati wa kukabidhiana rasmi shamba hilo lililoko Kilombero- Morogoro, kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali na SUMA-JKT mwishoni mwa wiki. **PICHA: OFISI YA MSAJILI WA HAZINA**

# HESLB yatoa bil. 99.9/- za mikopo awamu ya kwanza

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza 2021) orodha ya awamu ya kwanza yenye wanafunzi 37,731 wa mwaka wa kwanza waliopangiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 99.9 kwa mwaka wa masomo 2021/2022 unaotarajiwa kuanzia wiki ijayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema jana kuwa kati ya wanafunzi hao (37,731), wanaume ni 23,379 sawa na asilimia 62 na wanawake ni 14,352 sawa na asilimia 38.

Badru ameongeza kuwa HESLB imeanza kupeleka fedha za wanafunzi waliopangiwa mikopo katika vyuo mbalimbali na kuwataka wanafunzi kupata taarifa za kina katika akaunti walizotumia kuomba mkopo maarufu kama SIPA (Student's Individual Permanent Account) na kujiandaa kwenda vyuoni kwa ajili ya kujisajili.

"Serikali imeshatupatia fedha na tumeanza kuzipeleka vyuoni ... lengo letu ni kuhakikisha wanafunzi wanaopangiwa wanazikuta fedha vyuoni ambako watajisajili na kupokea ili watimize ndoto zao," alisema Badru.

Kuhusu kutangazwa kwa orodha ya Awamu ya Pili, Badru alisema imepangwa kutolewa Alhamisi, baada ya kukamilisha uchambuzi wa maombi unaoendelea na kuwataka waombaji mikopo kutembelea akaunti zao ya SIPA kupata taarifa kuhusu maombi yao.

"Orodha hii ya kwanza inajumuisha wanafunzi wenye sifa zikiwemo kuwa wahitaji, wameomba kwa usahihi na wana udahili wa chuo kimoja ... tunakamilisha uchambuzi wa maombi mengine na tutaoa orodha ya pili Alhamisi, Oktoba 21, 2021," alisema Badru.

Kwa mujibu wa Badru, serikali imetenga Sh. bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya jumla ya wanafunzi 160,000. Kati yao, wanafunzi 70,000 watakuwa ni wanufaika wapya na wanafunzi zaidi ya 90,000 ni wale wanaoendelea na masomo baada ya kufaulu mitihani yao ya mwaka.

Wakati huohuo, Badru alisema HESLB imeshapokea fedha kwa ajili ya malipo ya wanafunzi na taratibu za malipo zimeanza ili fedha hizo ziwe zimefika vyuoni kuanzia kesho.

Aidha, bodi iliwasihi kuwasihi waombaji wa mikopo kuwa watulivu wakati mchakato wa upangaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa kwa awamu inayofuata ukiendelea.

HABARI KITAIFA




Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda (katikati), akitoa maelekezo ya Mahakama ya Mwanzo Tarafa ya Kiponzero iliyohamishiwa Ifunda kurudi Kiponzero jana, wakati wa ziara yake katika mahakama hiyo, kushoto Diwani wa Kiponzero, Veny Myinga na Mbunge wa Kalenga, Jackson Kiswaga. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Serikali yaipatia SUMA JKT shamba la bil 152/-

**Na Mwandishi Maalumu**

SIKU chache baada ya kununua shamba lenye ukubwa wa hekta 5,818 kutoka kwa mwekezaji aliyeshindwa kuliendesha na kulipa madeni ya mikopo, serikali imelikabidhi shamba hilo kwa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA-JKT) kwa lengo la kulisimamia wakati ikiangalia namna bora ya kuliendeleza.

Serikali ilinunua shamba hilo lililopo Mngeta, Kilombero mkoani Morogoro baada ya kushinda zabuni iliyoendeshwa na Mfilisi (Msimamizi wa Muda), Silvanus Mlola aliyewekwa na Benki ya NMB iliyokuwa inamdai mwekezaji, Kampuni ya Kilombero Plantation Limited (KPL).

Akizungumza wakati wa makabidhiano yaliyofanyika shambani hapo jana, Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto alisema shamba hilo linakadiriwa kuwa na mali zenye thamani ya Sh. bilioni 152 na kulifanya kuwa miongoni mwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Ni dhahiri kuwa uwekezaji huu ni mkubwa na serikali inahitaji kupata mapato kutoka uwekezaji huu thabiti na endelevu.

Ni ukweli usiopingika kuwa wananchi wanaozunguka eneo hili watakuwa wanufaika wa kwanza wa mradi huu, na hivyo ni mategemeo ya serikali kuwa SUMA JKT itafanya kazi kwa bidii katika kuendeleza mradi huu ili kutimiza lengo la serikali.

"Hatutegemei kuona shamba linadorora na kurudi kule tulipolitoa, zaidi tunatazamia mwendelee kuboresha miundombinu lizalishe, muimarishe ulinzi kwenye mipaka inayozunguka shamba ili kuepusha uvamizi na migogoro ya ardhi na wananchi," alisema Mgonya.

Baada ya makabidhiano hayo, Mgonya ameielekeza SUMA JKT kuandaa Mpango wa Biashara utakaoonyesha nia na mikakati yao, ili uweze kuchambuliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Aidha, ili kulifanya shamba kujiendesha kwa tija, alisema baada ya uchambuzi wa mpango wa biashara na kubaini unafaa, Mamlaka inaweza kushauriwa kuundwa kwa kampuni tanzu chini ya SUMA JKT na serikali kupitia Msajili wa Hazina itakuwa na hisa kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shamba hilo.

"Lengo ni kutaka kuona kwa pamoja tunafikia malengo na matarajio ya serikali katika uwekezaji huu," alisisitiza Mgonya.

Akizungumzia wajibu na jukumu la Ofisi ya Msajili wa Hazina katika mradi huo, Mgonya alisema pamoja na majukumu mengine kama yalivyoanishwa katika kifungu cha 10 cha Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370, Ofisi ina jukumu la kuishauri serikali na kusimamia uwekezaji wake katika Taasisi, Mashirika na Wakala za Serikali.

Katika mradi wa shamba la Mngeta, Ofisi yake inatekeleza moja ya matakwa ya sheria, akisema walianza kwa kuishauri serikali kulinunua shamba hilo na kupendekeza Shirika la SUMA JKT ambalo pia linasimamiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina liwe mwendelezaji wa shamba la Kilombero.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa SUMA JKT, Brigedia Jenerali Absolomon Shausi ameishukuru serikali kwa hatua ya kulinunua na kuwakabidhi shamba hilo lenye manufaa makubwa kwa wananchi wa eneo linalozunguka na taifa kwa ujumla. Aidha, Brigedia Jenerali Shausi ameahidi kulisimamia na kuliendeleza shamba hilo ili kufikia malengo ya uwekezaji wa Serikali.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo ya makabidhiano, aliyekuwa Mfilisi wa Shamba hilo, Mlola ameishukuru Serikali kwa ushirikiano na kukamilisha kwa wakati makubaliano yote yaliyofikiwa katika zabuni husika mpaka kufikia hatua ya mwisho ya makabidhiano na hivyo kuahidi kutoa ushirikiano wakati wote.

## Mbaroni kisa madai Vitambulisho vya Taifa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia, Abdul Selemani (27), Mkazi wa Visiga Wilaya ya Kibaha kwa tuhuma za kutengeneza nyara za serikali.

Akizungumza na waandishi wa habari Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema Oktoba 12, mwaka huu, majira ya saa 11 jioni kwa kushirikiana na vyombo vingine walimkamata mtuhumiwa huyo anayedaiwa kutengeneza na kuuza Vitambulisho vya Taifa.

Kamanda Wankyo alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kuviuza vitambulisho hivyo kwa Sh. 10,000 kwa kila kitambulisho anachotengeneza.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na vifaa mbalimbali alivyokuwa anatumia ikiwamo vitambulisho viwili vya NIDA, kompyuta mpakato, Desktop kompyuta pamoja na Printer.

Kamanda Wankyo alisema upelelezi bado unaendelea juu ya tukio hilo na pindi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

Kadhalika, Kamanda Wankyo alisema tukio lingine lililotokea Oktoba 14, mwaka huu eneo la Kwamfipa Wilaya ya Kibaha, kwamba Jeshi la Polisi lilimtia mbaroni, Peter Baziro, kwa tuhuma za kuwatapeli watu kwa kuwauzia viwanja na kughushi hati za viwanja anavyoviuza na hati za mauzo.

Kamanda Wankyo alisema mtuhumiwa huyo pia amekuwa anadaiwa kutapeli watu na kujipatia fedha kwa kuwauzia magari.

Alisema hadi anakamatwa alikuwa amefanikisha kupata fedha kutoka kwa watu mbalimbali akiwamo, Jenifa Asa, aliyemlipa mtuhumiwa kiasi cha Sh. milioni 1.4 kwa lengo la kumuuzia eneo la ukubwa wa 20 kwa 20, huku akijua kwamba siyo kweli na hana eneo hilo.

Alisema mtuhumiwa huyo amekuwa akibadilisha majina kila anapofanya tukio la kutapeli ili asikamatwe.

# Mwanafunzi aozeshwa kwa mahari ya nguruwe

**Na Gurian Adolf, NKASI**

MKAZI wa Kitongoji cha Mabatini, wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Kennedy Fumpa (37), amekamatwa kwa tuhuma za kumuoa mwanafunzi wa darasa la tatu baada ya kulipa mahari ya Sh. 330,000 pamoja na nguruwe mmoja.

Mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 11 (jina linahifadhiwa), alikuwa darasa la tatu na alilazimika kuacha shule baada ya bibi yake aliyekuwa akimlea kupokea mahari hiyo hivi karibuni na mjukuu wake kuhamia kwa mwanamume huyo ili wakaanze maisha ya ndoa ya mume na mke. Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Godfrey Kalungwizi alisema serikali ya kijiji ilipata taarifa kutoka kwa uongozi wa shule kuwa mwanafunzi huyo amekuwa mtoro shuleni kwa muda mrefu ndipo jitihada za kumtafuta zikaanza. Alisema baada ya jitihada za uongozi wa kijiji kumtafuta mwanafunzi huyo na kumbana bibi aliyekuwa anamlea, alieleza kuwa alikwisha pokea mahari na mjukuu wake huyo tayari amekwisha olewa.

"Baada ya kufuatilia tulibaini wake kwa mahari ya Sh. 400,000, ambapo alipokea Sh. 330,000 taslimu na mnyama aina ya nguruwe mwenye thamani ya Sh. 70,000 na kukamilisha kiwango cha mahari alichopangiwa na kumchukua mwanafunzi huyo," alisema.

Naye Mwalimu Mkuu wa shule aliyokuwa akisoma mwanafunzi huyo, Josephat Joseph, alisema alikuwa haudhurii masomo na kwamba akaorodheshwa katika wanafunzi watoro wa muda mrefu mpaka uongozi wa shule ulipotoa taarifa kwenye serikali ya kijiji na kukamatwa akiwa tayari ameolewa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali, alithibitisha tukio hilo na kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo Oktoba 15 na kwamba polisi wanaendelea na uchunguzi na utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Alisema kisichokubalika ni kumbadilisha mtoto wa kike na nguruwe na sheria ya kumlinda mtoto ipo lazima ifuate mkondo wake.

HABARI KITAIFA

# Bil. 90/- za Uviko-19 mageuzi sekta ya utalii

**Na Gwamaka Alipipi**

SEKTA ya utalii nchini itafanyiwa maboresho makubwa na kuendeshwa kisasa hususani kwenye mbuga na hifadhi za wanyama, lengo ni kuinua utalii na kuifanya sekta hiyo kuendelea kuchangia katika uchumi na maendeleo ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano ya ugonjwa wa virusi vya corona katika Sekta ya Maliasili na Utalii, waziri wa wizara hiyo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema Sh. bilioni 90.2 za msaada walizoipokea zinakwenda kuleta mageuzi.

Dk. Ndumbaro alisema Wizara ya Maliasili na Utalii itajikita katika maeneo matano ambayo yameathirika zaidi kutokana na ugonjwa wa corona.

Aliyataja maeneo ya utekelezaji kuwa ni kuziwezesha taasisi za wizara zilizoathirika zaidi kutokana na mlipuko wa corona, ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Alisema Sh. bilioni 71.9 zimetengwa katika kuziwesha taasisi hizo ikiwamo kukarabati barabara katika maeneo ya hifadhi za Serengeti, Mkomazi, Tarangire, Nyerere, Kilimanjaro, Saadani na Gombe, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, misitu 10 ya hifadhi ya mazingira asilia chini.

Dk. Ndumbaro alisema: "Hatua hii itasaidia kufikika kwa urahisi kwa vivutio vya utalii na kukidhi kiu ya watalii na hivyo kuchochea shughuli za utalii na janga la corona".

Dk. Ndumbaro alitaja shughuli nyingine ni kuweka mifumo ya kielektroniki ya ufuatiliaji wa mashine kubwa na magari katika taasisi za uhifadhi. Shughuli nyingine ni kukarabati viwanja vya ndege nane katika hifadhi za Taifa za Serengeti, Nyerere, Tarangire, Mkomazi, Saadani na Katavi.

Alisema pia kutajengwa malango matano ya kupokelea wageni katika maeneo ya Likuyu Sekamaganga na Msolwa katika Hifadhi ya Nyerere, Hifadhi ya Mkomazi, Mapori ya Akiba ya Swagaswaga na Kijereshi.

Alisema kutafanyika ununuzi wa seti tano za mitambo ili kuwezesha ujenzi na ukarabati miundombinu katika hifadhi 13 za Taifa ambazo ni Serengeti, Ziwa Manyara, Mkomazi, Arusha na Kilimanjaro, Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa, Rumanyika-Karagwe, Kigosi na Rubondo na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Tarangire na Nyerere.

Dk. Ndumbaro alisema pia zitanunuliwa boti maalum yenye kioo kwa ajili ya utalii wa baharini itakayotumika katika eneo la Kilwa Kisiwani.

Pia, alisema kutafanyika ukarabati wa miundombinu ya utalii ikiwamo barabara na vituo vya taarifa za watalii katika mapori ya akiba 11 na mapori tengefu sita kwa ajili ya kuendeleza utalii wa picha.

Alisema pia kutanunuliwa seti za mitambo ya kujenga na kukarabati miundombinu katika maeneo ya pori tengefu la Kilombero na mapori ya akiba ya Mkungunero na Moyowosi, kwamba mitambo hiyo itahusisha ununuzi wa gari moja la kuchimba visima, ununuzi wa boti maalum ya kufanya doria mashine za kuchimba visima.

Alisema shughuli nyingine ni kuweka mifumo ya kielektroniki ya kutambua, kuhakiki na kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora;

Mbali na hilo, alisema kutatolewa mafunzo kwa wataalamu wa tathmini, wakufunzi, walimu wa wakufunzi, watoa huduma za malazi katika kupanga daraja za ubora.

"Tutaboresha miundombinu ya mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato inayowezeshwa na mkongo wa Taifa, ununuzi wa mifumo kwa ajili ya miundombinu ya TEHAMA.

Dk. Ndumbaro alisema pia kutanunuliwa magari matatu kwa ajili ya kazi za udhibiti wa ubora na kujenga uelewa wa miongozo ya udhibiti wa corona.

Waziri Ndumbaro alisema fedha hizo pia zitaelekezwa katika kuimarisha masoko na kutangaza utalii.

Alisema kutafanyika ukarabati wa vituo saba vya urithi wa kiutamaduni vya Mikindani Mtwara, Tendaguru-Lindi, Magofu ya Kua-Mafia, Msikiti wa Mbua Maji Mbweni, Makaburi na Msikiti wa Bandarini na Kimbiji- Dar es Salaam.

Pia kutafanyika ujenzi wa kituo cha kutolea taarifa za utalii katika Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato katika lango la Meja Jenerali Kijuu.

Alisema kutanunuliwa vifaa kwa ajili ya kituo cha kutolea taarifa za utalii kidigitali, ili kuwezesha utangazaji wa utalii kwa kutumia mitandao ya kijamii.

Dk. Ndumbaro alitaja eneo lingine ni kuimarisha mazingira ya biashara ya utalii kwa kuzingatia viwango vya afya na usalama vya kitaifa na kimataifa.

Alisema eneo lingne ni kushirikisha sekta binafsi kwa kuwajengea uwezo wa kukabiliana na corona.



Faraja Mwakifuna (kulia), mzalishaji na msambazaji wa lishe mbadala kutoka Kampuni ya BF Suma akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mnkunda, alipotembelea maonyesho yaliyoandaliwa na Shirika la Jatu kupitia kampeni ya 'Anza na Ekari Moja' yaliyofanyika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma juzi. **PICHA PETER MKWAVILA**

# CHADEMA yazungumzia hukumu ya Sabaya

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, amesema kuna haja ya kufanya marekebisho ya Katiba, ili kuhakikisha viongozi waliopo madarakani wanashtakiwa pale wanaposababisha madhara kwa raia.

Mnyika alitoa kauli hiyo wakati akizungumzia hukumu iliyotolewa mwishoni mwa wiki kwa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya kwenye tukio la uzinduzi wa Siku ya Utu iliyoandaliwa na Chama cha NCCR-Mageuzi lililofanyika Dar es Salaam jana.

Alisema Katiba mpya ndio itawapatia Watanzania utu, haki, uhuru na maendeleo endelevu hususani yanapokuja masuala magumu katika taifa.

"Hukumu ya Sabaya ni kielelezo hususani waliopo kwenye nafasi za kiuongozi, wasidhani kwamba wanaweza kukwepa hukumu. Kwa hiyo tukio la Sabaya na mabaya yake na hatua mbaya zilizochukuliwa dhidi yake iwe fundisho kwa wengine," alisema Mnyika.

"Lakini tukio hili lisirudishe nyuma kila mmoja, lisichukuliwe kwamba sasa taifa letu ndio limefika katika ulimwengu wa haki, ulimwengu wa haki na utu wa mazingira kwa wanawake, vijana na kwa kila kundi katika jamii kwa nchi tuliyokubali demokrasia utapatikana kukiwa na mifumo huru ya bunge huru, mahakama huru, taasisi huru na tusiwe na sheria mbaya."

"Na hata kiongozi anapotenda matendo kama yale tusisubiri mpaka watu waumizwe kwa muda mrefu, ndiyo uwajibikaji uwezekane. Na kwa kuwa wakati anahojiwa alisema alitumwa na mamlaka za juu, ni lazima tubadili Katiba ya nchi yetu ili kupunguza madaraka ya mamlaka za juu ikiwamo mamlaka ya Rais. Kwa hiyo ni rai yangu kuwa hatua za kurejeshwa utu zifanyike."

Sabaya na wenzake wawili walitiwa hatiani na Mahakakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha na kumhukumu kifungo cha miaka 30 jela.

## Mara yapata bil. 14/- za ujenzi madarasa

**Na Mobini Sarya,** TARIME

MKOA wa Mara umepokea zaidi ya Sh. bilioni 14 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya sekondari 600 na bweni moja la wanafunzi wenye mahitaji maalumu pamoja na madawati, kutoka mpango wa kupambana na na Uviko-19.

Mkuu wa Mkoa, Ally Hapi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea halmashauri za mkoa huo kwa ajili ya kuunda kamati kusimamia ujenzi wa madarasa hayo kwa kipindi cha miezi miwili.

Akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Rorya na Tarime, Hapi alisema maandalizi ya kujenga madarasa hayo na vituo sita vya afya mkoani humo yameanza aliwataka wakurugenzi kuunda kamati hizo haraka na kuzipatia semina.

"Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa mitano iliyopatiwa pesa nyingi kuliko mikoa mingine, tulikuwa na upungufu wa madarasa 618 tutajenga yote ikiwamo bweni moja la watoto wenye mahitaji maalumu na vyumba 300 vya shule shirikishi na kila darasa limetengewa Sh. milioni 20," alisema Hapi

Akikagua ujenzi wa kituo cha afya Nyamagaro, tarafa ya Nyancha wilayani Rorya ambacho kimetengewa Sh. milioni 250 kutokana na fedha za tozo ya simu.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONYESHA NIA: USIMAMIZI WA PROGRAMU YA KUREJESHA USTAWI WA MAISHA KUMBUKUMBU 0010007128

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kutekeleza programu ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha kwa kaya zilizoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale

katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

### MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA

Kampuni inahitaji mkuza wa ardhi pamoja na maeneo ya vituo kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa shughuli za bomba la mafuta. Mchakato wa utwaaji wa ardhi umefanyika kwa kuzingatia sheria za nchi ya Tanzania pamoja na matakwa ya Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Utoaji wa ardhi mbadala ya kilimo na makazi kwa watu walioguswa na Mradi (PAPs) na msaada wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha vinatolewa kwa Kaya zilizoguswa na Mradi.

Kulingana na mipango ya juu ya programu ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha ulivyoelezwa kwenye Mipango tisa ya hatua za Mpango Kazi wa Makazi Mapya (RAPs) (moja kwa kila mkoa na moja kwa kila ''Eneo la Kipaumbele '' au maeneo ya kambi 12 na karakana ya kuandalia mabomba), Mradi unatafuta taasisi mshirika ya Kitanzania yenye weledi, uzoefu na uwezo wa kusaidia usimamizi na utekelzaji wa programu ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha kwa takribani Kaya 400 zilizoguswa na ukanda wa bomba la mafuta pamoja na baadhi ya vituo vya huduma.

Mawanda haya hayajumuishi ''Maeneo ya Kipaumbele'' au kambi na karakana ya kuandalia mabomba pamoja na eneo la kuhifadhi vifaa lililopo ukanda wa bahari katika Rasi ya Chongoleani.

Mawanda ya huduma yanahitaji utekelezaji wa vipengele saba (7) muhimu vya programu ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha kama ilivyoelezwa kwenye Mpango Kazi wa Uhamishaji watu na Makazi:

1. Maandalizi ya Ardhi na Upandaji Mazao katika Ardhi Mbadala ya Kilimo (LRA1),
2. Mpango wa Uboreshaji wa zao la Mahindi (LRA2),
3. Mazao Mseto (LRA3),
4. Uzalishaji wa Kuku (LRA 4),
5. Uzalishaji wa Mifugo (LRA5),
6. Ufugaji wa Nyuki (LRA 6),
7. Uendelezaji wa Biashara (LRA 7).

Programu hizi zinahitaji kuundwa na kutolewa kwa namna ambayo itaendana na muktadha wa maeneo husika, na kwa kiwango kinachowezekana na utekelezaji wa programu hizi pia uzingatie mapendekezo ya kaya husika. Haitarajiwi kwamba programu hizi zitatekelezwa katika jamii zote. Mawanda ya huduma yatahitaji uwepo wa wafayakazi katika eneo la Mradi kwa shirika litakalochaguliwa pamoja na kushirikiana na wadau wa ndani pamoja na Kaya chini ya usimamizi na muongozo wa mfanyakazi wa kampuni ya EACOP.

### VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana moja kwa moja na Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa:
  - Kutekeleza programu za urejeshaji, uboreshaji au uendelezaji wa Ustawi wa Maisha kwa jamii za vijijini.
  - Utekelezaji wa programu za aina hiyo kwa viwango vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania.
  - Kusimamia miradi mikubwa na wakandarasi washirika.
  - kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
  - Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
  - **Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuoneshania ya kutekeleza shughuli za progamu.**

Mawanda haya yanaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **26 Octoba 2021.**

**Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.**

2165188502

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONYESHA NIA: USIMAMIZI WA PROGRAMU YA KUREJESHA USTAWI WA MAISHA KUMBUKUMBU 0010007129

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kutekeleza programu ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha kwa kaya zilizoguswa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231.

### MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA

Kampuni inahitaji mkuza wa ardhi pamoja na maeneo ya vituo kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa shughuli za bomba la mafuta. Mchakato wa utwaaji wa ardhi umefanyika kwa kuzingatia sheria za nchi ya Tanzania pamoja na matakwa ya Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Utoaji wa ardhi mbadala ya kilimo na makazi kwa watu walioguswa na Mradi (PAPs) na msaada wa Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha vinatolewa kwa Kaya zilizoguswa na Mradi.

Kulingana na mipango ya juu ya programu ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha ulivyoelezwa kwenye Mipango tisa ya hatua za Mpango Kazi wa Makazi Mapya (RAPs) (moja kwa kila mkoa na moja kwa kila ''Eneo la Kipaumbele '' au maeneo ya kambi 12 na karakana ya kuandalia mabomba), Mradi unatafuta taasisi mshirika ya Kitanzania yenye weledi, uzoefu na uwezo wa kusimamia utekelezaji wa programu ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha kwa kaya Zaidi ya 8000 zilizoguswa na Mradi katika jamii zote zilizopitiwa na Mradi huo kwenye eneo lote la mkuza wa bomba lililopo Tanzania.

Mawanda hii haijumuishi ''Maeneo ya Kipaumbele'' au kambi na karakana ya kuandalia mabomba pamoja na eneo la kuhifadhi vifaa lililopo ukanda wa bahari katika Rasi ya Chongoleani.

Mawanda ya huduma yanahitaji utekelezaji wa vipengele saba (7) muhimu vya programu ya Urejeshaji wa Ustawi wa Maisha kama ilivyoelezwa kwenye Mpango Kazi wa Uhamishaji watu na Makazi:

1. Maandalizi ya Ardhi na Upandaji Mazao katika Ardhi Mbadala ya Kilimo (LRA1,
2. Mpango wa Uboreshaji wa zao la Mahindi (LRA2),
3. Mazao Mseto (LRA3),
4. Uzalishaji wa Kuku (LRA 4),
5. Uzalishaji wa Mifugo (LRA5),
6. Ufugaji wa Nyuki (LRA 6),
7. Uendelezaji wa Biashara (LRA 7).

Programu hizi zinahitaji kuundwa na kutolewa kwa namna ambao itaendana na muktadha wa maeneo husika, na kwa kiwango kinachowezekana, utekelezaji wa programu hizi pia uzingatie mapendekezo ya kaya husika.

Haitarajiwi kwamba programu hizi itatekelezwa kwenye jamii zote.

Mawanda ya huduma yatahitaji uwepo wa wafayakazi katika eneo la Mradi kwa shirika litakalochaguliwa pamoja na kushirikiana na wadau wa ndani pamoja na Kaya chini ya usimamizi na muongozo wa mfanyakazi wa kampuni ya EACOP. Mawanda hii inaweza kugawanywa kimkoa au kiutalaam na KAMPUNI inaruhusu Wazabuni kuwasilisha pendekezo kwa ajili ya kipengele kimoja, kadhaa au vyote

### VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA

Taasisi zitakazoonesha nia yanaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana moja kwa moja na Urejeshaji wa ustawi wa maisha.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kutekeleza programu za urejeshaji, uboreshaji au uendelezaji wa Ustawi wa Maisha chini ya sheria ya Tanzania kwa jamii za vijijini au utekelezaji wa programu za aina hiyo chini ya sheria za Tanzania na matakwa ya Mashirika ya Kifedha ya Kimataifa kwa ajili ya miradi mikubwa ya miundombinu nchini Tanzania; Uzoefu na uwezo wa k usimamia programu kubwa; kuhusisha na kusimamia washirika pamoja na kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali za mitaa na sekta binafsi.
- Wafanyakazi waliopendekezwa kufanya kazi kwenye Mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
- **Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za programu.**

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **26 Octoba 2021.**

**Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.**

2165188502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi wetu michuano CAF jipangeni inawezekana

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, Biashara United na Azam FC, tayari wamemaliza dakika 90 za kwanza nyumbani baada ya kushuka dimbani Ijumaa na Jumamosi.

Biashara United ambayo Ijumaa iliikaribisha Al Ahli Tripoli ya Libya katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kupata ushindi wa 2-0, sasa itahitaji sare yoyote ama kutopoteza kwa zaidi ya mabao hayo watakaporudiana ugenini Jumamosi wiki hii.

Lakini kwa upande wa Azam FC ambayo ililazimishwa sare tasa na Pyramids FC ya Misri katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salam, yenyewe ina mlima mrefu kidogo Jumamosi wiki hii itakapokuwa nyumbani kwa Wamisri hao.

Ushindi ama sare yoyote ya mabao ndivyo vinavyohitajika kwa Azam FC ili kuipa tiketi ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoshika nafasi ya pili kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mujibu wa kanuni za michuano hiyo, timu zitakazopata matokeo ya jumla katika hatua hii, zitasubiri kupangiwa kucheza mechi ya moja ya mtoano nyumbani na ugenini dhidi ya timu zitakazotolewa raundi ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa ili kusaka tiketi ya kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Tunatambua haitakuwa rahisi kwa wawakilishi hao wa Tanzania ambao wanahitaji kupata matokeo ili kusonga mbele, hasa ikizingatiwa na ubora wa wapinzani wao.

Lakini tunaamini kama watajipanga vema kuanzia sasa hadi mwishoni mwa wiki kabla ya mechi hizo za ugenini, inawezekana kabisa kwa Azam na Biashara United kupata matokeo chanya na kusonga mbele.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba tayari wamefahamu ubora na udhaifu wa wapinzani wao, hivyo kinachotakiwa ni kufanyia kazi udhaifu wao na kwenda kujitoa kiume mwanzo mwisho wa mchezo.

Kwa Biashara United, inapaswa kutokubweteka kwa matokeo chanya iliyoyapata katika mchezo wa awali nyumbani, na badala yake inatakiwa kwenda kushuka uwanjani ikisaka ushindi kama vile haikushinda awali.


Kadhalika, kwa Azam FC, inafaida kubwa kwa kutokukubali kuruhusu bao nyumbani, hivyo inachotakiwa kukifanya ni kwenda kuhakikisha inauanza mchezo huo kwa kasi na kutafuta bao la ugenini la mapema ili kuwapa wapinzani mzigo mrefu na kuwaongezea presha ya mchezo.

Nipashe hatuna shaka kabisa kwa wawakilishi wetu kwenda kumaliza kazi ugenini endapo tu watafanyia kazi kasoro ndogondogo zilizojitokeza katika mechi zao za awali na kutambua dhamana kubwa waliyoibeba ya kuipeperusha bendera ya Tanzania kimataifa.

Si hilo tu, wachezaji wote wa timu hizo za Tanzania wanapaswa kutambua kuwa hii ni michuano muhimu kwao kwa kuitumia kama daraja la kwenda kutangaza soko lao kimataifa na hatimaye kupata klabu kubwa zaidi Afrika na hata Ulaya.

Hii ni kutokana na michuano hiyo kutupiwa jicho zaidi na mawakala mbalimbali duniani na kila msimu imekuwa tiketi kwa wachezaji wengi kununuliwa na klabu kubwa ndani na nje ya bara la Afrika, hivyo ni wakati wa kila mchezaji kujitoa kufa kupona kwa kutambua yapo maslahi makubwa kwao kwa klabu yao kusonga mbele kwani wanaongeza wigo mpana wa soko lao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Motisha Biashara usiishie vs Simba, inahitaji nauli kuifuata Al Ahli Tripoli

**NIMEWASIKIA** baadhi ya viongozi wa Biashara United wakisema kuwa hali ya kifedha kwenye klabu yao kwa ajili ya kwenda kucheza mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika ni mbaya.

Wakizungumza kwenye vipindi mbalimbali vya michezo, viongozi hao wamewaomba wadau mbalimbali kuwasaidia ili kuweza kumudu gharama za kwenda kucheza mechi ya marudiano dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya.

Kuna uwezekano mkubwa mechi hiyo isichezwe nchini Libya kutokana na hali ya kisiasa, badala yake huenda ikachezwa nchini Tunisia. Timu inahitaji nauli, posho za wachezaji, maandalizi na hata gharama za kuiwezesha kuishi ikiwa nje ya nchi.

Kwa jinsi ambavyo viongozi wa Biashara United wanavyosema, kama wasipopata sapoti ya wadau, hali inaweza kuwa mbaya. Ikumbukwe wawakilishi hao wa Tanzania kwenye michuano hiyo, wameshinda mechi yao ya kwanza mabao 2-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na wanahitaji ushindi, sare yoyote, au kufungwa goli lisilozidi moja, ili kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Kama ni uzalendo, huu ndiyo wakati wa kuuonyesha, kwani Biashara United ikishinda sifa itakwenda kwa Tanzania nzima na si mkoa wa Mara peke yake. Ni nani mpaka sasa anaweza kusaidia kulinda ushindi wa Biashara United kwa kutoa pesa ili kuiwezesha kwenda ugenini kufanya vizuri na kutoa motisha kwa wachezaji pia?

Nilishangazwa kwa baadhi ya wanasiasa kuja kwa kasi wakati Ligi Kuu Tanzania imeanza kuziahidi timu za mikoani mwao mamilioni ya shilingi zikishinda.

Biashara United iliahidiwa kiasi cha shilingi milioni 15 ikishinda mechi yake dhidi ya Simba, huku sare yoyote ikiahidiwa shilingi milioni 10. Wachezaji wa timu hiyo walipata na kugawana pesa ambazo walipewa wakati timu ikitoa sare dhidi ya Simba. Dodoma nako, timu ya Dodoma Jiji iliahidiwa hivyo hivyo. Bahati mbaya ikafungwa.

Ahadi wala si kitu kibaya, lakini inashangaza kuona wanasiasa walioiahidi Biashara United ilipocheza dhidi ya Simba, wako kimya. Sijasikia hata wakipewa japo shilingi milioni tano tu, iliposhinda mechi ya Kombe la Shirikisho dhidi ya Al Ahli Tripoli. Ni kama hakuna kilichotokea.

Hivi tayari viongozi wa Biashara United wameshaanza kuhaha, lakini bado kumekuwa na ukimya kwa wanasiasa wale wale walioiahidi Biashara United ikicheza na Simba.

Hakika inashangaa! Hivi mechi dhidi ya Simba ilikuwa muhimu zaidi kuliko hii ya kimataifa?

Na kama wanasiasa hasa Wakuu wa Mikoa kwa sasa wameanza kujitokeza kuzisaidia timu za mikoa yao, inakuaje wasijitokeze kusaidia kidogo walichonacho na kuibeba Biashara United?

Wasipofanya hivyo, kuna baadhi wataanza kuunganisha 'doti'. Kwa nini wanasiasa hawa walitoa ahadi kwenye mechi dhidi ya Simba tu? Mbona kwenye mechi zingine tena za kimataifa kama hizi, ahadi huwa hakuna? Mbona kuna timu zimecheza mechi za Ligi Kuu bila timu pinzani kuahidiwa chochote?

Kama ni hamasa, kwa nini Biashara United hao hao wasipewe hamasa waliposhinda, au kwa ajili ya mechi ya marudiano?

Ninasema haya kwa sababu kama Biashara United ikiachwa nje ya nchi ikiwa haina pesa za kutosha, kuna uwezekano mkubwa wa kutolewa kwenye michuano hii, licha ya ushindi ilioupata.

Mara nyingi timu za Afrika ya Kaskazini, maarufu kama za 'Waarabu', lakini michuano hii ya kimataifa, imekuwa na figisu nyingi, hivyo ni uwezo wa kipesa pekee, ndiyo utakaoifanya timu hiyo kuepuka kukaribishwa kinafiki na wenyeji. Kupewa hoteli badala ya kukodi wenyewe. Kula vyakula vya huko, wakati kwa sasa timu zote ambazo zimekomaa kwenye michuano hiyo huondoka na vyakula na wapishi wao. Biashara United itashindwa hata kukodi basi, na kuingia kwenye mtego wa kupewa basi na wenyeji, vitu ambavyo kwa sasa vimekuwa vinaepukwa sana na timu zenye uzoefu kwenye michuano hiyo.

Nawakumbusha tena, wanasiasa waliokuwa wanaahidi timu za mikoa yao zikishinda, huu sasa ndiyo wakati wa kuisaidia Biashara United. Huu ndiyo wakati wa kuonyesha uzalendo wa kweli kwa nchi ya Tanzania.

Waliotoa motisha Biashara United wanapaswa kulimulika hili ili kuondoa minung'uniko iliyotolewa awali na mashabiki wa Simba wakidai huenda kuna mkono wa wapinzani wao wanaoupitishia kwa wanasiasa, wakihoji kwa nini ahadi hizo zinatolewa tu wakati wanapocheza dhidi ya timu yao!

# Risiti za EFD zawapeleka mahakamani

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA 12 wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamefikishwa mahakamani kwa kosa la kuuza bidhaa bila kutoa risti za kieletroniki (EFD) pamoja na kuzuia maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) kutekeleza majukumu yao.

Watuhumiwa hao walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama na kusomewa mashtaka yao mbele ya hHakimu David Msalilwa.

Miongoni mwa washtakiwa hao waliofikishwa mahakamani ni pamoja na mmiliki wa Hoteli ya River Mark, Joseph Wabani ambaye alisomewa shtaka lake na kukiri na kuhukumiwa kwenda jela mwezi mmoja ama kulipa faini ya Sh. milioni 1.5.

Kwa upande wake, Hakimu Mkazi wa Wilaya Kahama, Donacian Agustino, aliyesikiliza kesi ya mtuhumiwa Lucas Kishimbe anayemiliki duka la bidhaa za jumla na usafirishaji, alimhukumu mshtakiwa huyo kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini Shilingi milioni tatu baada ya kukiri kosa lake.

Watuhumiwa wengine kesi zao zitaendelea kusikilizwa leo katika mahakama hiyo.

Meneja wa TRA, Warioba Kanire, akizungumza na waandishi wa habari, alisema wameanza kuchukua hatua za kisheria kwa wafanyabiashara wanaokaidi agizo la kutumia EFD katika biashara zao.

Kanire alisema kuwa baadhi ya wafanyabiashara wanatoa risiti zenye thamani pungufu ya kiasi cha fedha walichopokea na kuzuia maofisa wa TRA kutekeleza majukumu yao na wengine wakiitwa ofosini kwake wanakataa kufika.

Alisema TRA imekuwa ikitoa elimu kila mara ya ulipaji wa kodi kwa wafanyabiashara waliopo wilayani Kahama, lakini wengi wao wanakaidi kufuata maelekezo hali inayosababisha serikali kukosa mapato yake.

Kanire alisema jumla ya wafanyabiashara 12 wamefikishwa mahakamani kwa makosa ya kutokuwa na mashine za EFD huku wengine wakitoa risiti zenye upungufu wa fedha wanapouza bidhaa.

Alizitaja baadhi ya kampuni zilizofikishwa mahakamani kuwa ni pamoja na Magnam Resources, Submarine Hotel, Kitapela Investment, Chillers Night Club, Emmanuely Kidenya, Juma Daud Saguda, Cosmas Joachim Mushi, Ushirombo Phamas, bernad Kalamu Lyaka, Rivermak Hotel, Steven Mathias Masunga na Adelina Sylivester Mallya.

# Serikali yawahakikishia viwanda vya nguo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, amesema serikali inaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Pamba hadi Nguo (C2C) kupunguza uuzaji wa pamba ghafi nje ya nchi kutoka asilimia 70 kwenda 50.

Lengo ni kuviwezesha viwanda vya uzalishaji nguo nchini kupata pamba ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji nguo kulingana na mahitaji ya soko.

Waziri Prof. Mkumbo aliyasema hayo alipotembelea Kiwanda cha Kuzalisha nguo cha NIDA kilichoko Tabata, jijini Dar es Salam juzi.

Katika kufungamanisha bidhaa za kilimo na viwanda vya uzalishaji, Prof. Mkumbo aliwaasa wamiliki wa viwanda vya kuzalisha nguo nchini kununua pamba ghafi ya wakulima inayolimwa katika mikoa 17 nchini kwa bei nzuri ili kuwavutia wasiuze pamba hiyo nje ya nchi bali wawauzie wao ili kukidhi mahitaji ya pamba ghafi katika viwanda vyao. Aidha, Prof. Mkumbo alisema serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ikiwamo urekebishaji wa sheria mbalimbali hasa inayohusu ajira kwa wageni viwandani kuwa mgeni 1 kwa Watanzania 10 na kutoka miaka 5 hadi 8 ili kurahisisha undeshaji wa mitambo inayotumia teknolojia ya kisasa na kuhuisha teknolojia ya uendeshaji mitambo hiyo kwenda kwa Watanzania.

Prof. Mkumbo pia alisema serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kuhakikisha viwanda vinavyozalisha nguo vipate pamba ya kutosha kukidhi mahitaji yake ya pamba ghafi kwa ajili ya uzalishaji nguo nchini.

Naye Meneja wa Uhusiano na Ushauri wa Kisheia wa Kiwanda cha NIDA, Rajabu Honello, alisema serikali iendelee kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini kwa kulinda bidhaa za viwanda zinazozalishwa nchini kwa kuwa viwanda hivyo vinatoa ajira nyingi na kuchangia katika pato la taifa wakati ikilinda wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa kutoka nje ya nchi. Mingoni mwa viwanda alivyotembelea Waziri Mkumbo ni cha kuzalisha bidhaa za umeme cha Africab kilichopo Kurasini na kiwanda cha NIDA ambacho kinazalisha bidhaa mbalimbali za nguo. Viwanda hivyo vinauza bidhaa zake Afrika.



Mratibu wa Chama cha Wazazi Wenye Watoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHT), Hidaya Alawi, akizungumza katika kikao cha wanachama wa chama hicho, jijini Dar es Salaam juzi, walipokutana kujadili maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Watoto wenye Ulemavu huo ambayo yanatarajiwa kufanyika Oktoba 25, mwaka huu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# NMB yatoa vifaa vya mil. 180/- elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Mteja Benki ya NMB imetoa vifaa mbalimbali vya ujenzi, na samani kwenye sekta ya elimu kwa shule za msingi na sekondari ikiwamo vifaa vya afya katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Simiyu, Iringa, Rukwa, Mara, pamoja na Kilimanjaro.

Katika kuadhimisha wiki hiyo ambayo ilianza Oktoba 3, 2021 ikiwa na kauli mbiu Nguvu ya Huduma (The Power of Service), benki hiyo imetoa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 180.25 lengo likiwa kuunga mkono juhudi za serikali kuboresha sekta ya elimu na afya.

Katika mkoa wa Dodoma, Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alikabidhi viti 200 na meza 200 kwa ajili ya shule za sekondari za Nondwa, Msisi Juu na Bahi za Wilaya ya Bahi na Shule ya Sechelela katika Jiji la Dodoma.

Mtendaji mkuu huyo wa NMB akikabidhi vifaa hivyo kwa mkuu wa mkoa huo, Anthony Mtaka, alisisitiza ushirikiano wa benki hiyo na wananchi katika utoaji huduma utaendelea kuimarika nchi nzima.

Zaipuna alikabidhi pia madawati 50 kwa Shule ya Msingi Chiguluka, mabati ya kuezekea Sekondari ya Bahi na vifaa vya hospitali kwa zahanati za Chimendeli na Hospitali ya Wilaya Bahi na kuzindua hati ya kiapo cha huduma kwa wateja ikilenga kutoa nafasi kutoa huduma kwa saa 24.

Mtaka aliomba NMB kuendelea kuangalia na makundi mengine yenye uhitaji hasa wanawake na kwamba wasione shida wanapoombwa misaada kwani kinachowaponza ni ukubwa wao ukilinganisha na benki zingine nchini.

Mkoani Mara NMB imetoa msaada wa madawati 100 yenye thamani ya zaidi ya Sh. 10 milioni kwa Shule ya Msingi Kiriba iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma vijijini.

Msaada huo umesaidia kumaliza kabisa tatizo la upungufu wa madawati, lilokuwa likiikabili shule hiyo kwa muda mrefu na kueplekea baadhi ya wanafunzi kukaa chini wakati wa vipindi.

Mkoani Kilimanjaro benki hiyo imetoa vifaa mbalimbali vya elimu kwenye shule za sekondari wilayani Moshi mkoa humo vyenye thamani ya Sh. milioni 40 ikiwa ni sehemu kurejesha sehemu ya faida kwa wateja wake na kuunga mkono juhudi za serikali kuinua sekta ya elimu nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Said Mtanda, akipokea vifaa hivyo ambavyo ni madawati na vifaa vya kuezekea, alisema mchango wa benki ya NMB utaendelea kuuenzi kwasababu unasaidia kupunguza changamoto za sekta ya elimu.

Shule zilizonufaika na vifaa hivyo ni Shule ya Msingi Mawalla, Shule ya Sekondari Mwika, Shule ya Sekondari Mangoto, Shule ya Sekondari Mieresini na Shule ya Sekondari Himo Sekondari zilizochangiwa mabati 293 na madawati 300 kwa ajili ya kuboresha mazingira ya masomo kwa wanafunzi.

Mkoani Arusha Benki hiyo imetoa vifaa mabati, madawati, vitanda, viti na meza wa shule mbalimbali kutoka Wilaya za Arusha mjini, Arusha Vijijini, Karatu Meru Vijijini pamoja na Monduli Vijijini vikiwa na thamani ya Sh. milioni 45.

Katika Mkoa wa Simiyu benki hiyo imetoa madawati, meza na viti, mabati pamoja na mbao kwa ajili ya shule nne za msingi na Sekondari katika Wilaya ya Maswa vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 24.

Akikabidhi vifaa hivyo Meneja Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema kuwa NMB imetoa vifaa hivyo ili kuhakikisha mazingira ya wanafunzi kusomea yanakuwa mazuri ili watoto waweze kufikia malengo yao.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Aswege Kaminyoge, akipokea vifaa hivyo aliishukuru benki hiyo, huku akiwataka walimu na wanafunzi kuhakikisha vifaa hivyo vinatunzwa kwa makini ili kuweza kukaa muda mrefu.

Katika Mkoa wa Iringa Benki hiyo imetoa madawati 50 kwa shule ya msingi Itunduru yenye thamani ya Sh. milioni tano, huku Mkoani Rukwa katika shule ya msingi Mfaranyaki ikitoa mabati 200 yenye thamani ya Sh. milioni 6.25.

Morogoro, pia imetoa vifaa vya afya kwa ajili ya hospitali mpya ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro vyenye thamani ya Sh. milioni 10.

# Zebaki inavyoathiri kiafya wachimbaji Kanda ya Ziwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema asilimia kubwa ya wagonjwa wa saratani walioko Hospitali ya Ocean Road jijini Dar es Salaam wanatoka Kanda ya Ziwa.

Amesema, wagonjwa hao wanaonekana wamethiriwa na kemikali inayotumika kukamatia madini ya dhahabu (zebaki). Jafo aliyabainisha hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Biashara, Viwanda na Mazingira katika mdogo mdogo wa madini ya dhahabu uliopo Kcha Mwime, Kata ya Zongomela Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga.

Alisema kuwa wachimbaji wadogo wamekuwa wakitumia kemikali kukamatia madini ya dhahabu bila kufuata utaratibu za kiafya kwa kutokuvaa vifaa vya kulinda afya zao wakati wa uchenjuaji wa madini hayo hali ambayo inasababisha kuonekana kuwa na maradhi ya saratani. Aliwataka kuacha tabia ya kununua kemikali hizo kama bangi na badala yake wafuate utaratibu wa ununuzi kemikali hizo kupitia Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na kuchukua tahadhari wakati wa matumizi ili kuondokana na madhara ambayo hujitokeza.

Awali Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo Mkoa wa kimadini Kahama, Joseph Nalemi, alisema kwa sasa wananunua dawa za kukamatia zebaki kama bangi kwa sababu hakuna ofisi maalumu ya kuuzia krmikali hizo na hata utunzaji wake wanatunza bila tahadhari.

Alisema awali walikuwa wakinunua kilo moja ya zebaki kwa Sh. 250,000 hadi 300,000, lakini kwa sasa imekuwa adimu kupatikana, hivyo wananunua kwa Sh. 450,000 na kwamba kungekuwa na sehemu ya kununua dawa hizo wangenunua kwa bei halali, na kupata elimu ya namna ya matumizi na utunzaji.

Naye mmoja wa wachimbaji wadogo wa mgodi huo, Fredy Fikili, alisema kuwa wamekuwa wakipata madhara makubwa wakati wa uchomaji wa dhahabu kwa kutumia maji ya mkaa kabla ya kupeleka sokoni, hali ambayo inasababisha kuvuta mvuke wenye sumu ya dawa na kupata satarani baadaye.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Biashara, Viwanda na Mazingira, David Kihenzile, alisema matumizi mabaya ya zebaki yanaweza kuathiri kizazi hadi kizazi, hivyo aliwataka kuangalia jinsia ya kupambana na athari za matumizi ya zebaki na kulinda afya zao.

Kihenzile aliwataka wachimbaji hao kutunza mazingira yanayowazunguka ikiwamo kutumia vema matumizi ya dawa zakukamatia dhahabuzebaki ili kufanya shughuli za uchimbaji wa wakiwa na afya njema na kuhakikisha hawatoroshi madini yanayopatikana.



Mmoja wa wachimbaji wadogo katika mgodi wa Mwime ulioko Kata ya Zongomela, Manispaa ya Kahama, akiwaonyesha wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Biashara, Viwanda na Mazingira namna wanavyoosha mchanga unaosadikiwa kuwa na madini kwa kutumia kalai na zebaki wakati wa ziara ya kukagua athari za kemikali hiyo katika mgodi huo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# NCCR-Mageuzi yataka serikali kuanza ukurasa mpya

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimesema ili taifa lisonge mbele kuna haja ya serikali iliyopo madarakani kuanza ukurasa mpya na kuacha yaliyoleta madhara kwa wananchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana Dar es Salaam na Mwenyekiti wake, James Mbatia, wakati wa uzinduzi wa siku ya utu iliyoandaliwa na chama hicho.

"Namwomba Rais Samia kama ambavyo alitamka hadharani kwamba hataki dhuluma zozote zile na ili tuenzi hali ya utu leo, ni vyema madhira yote ambayo serikali ya sasa imeyarithi huko iachane nayo ili taifa lisonge mbele na lizaliwe upya, liweze kuwa nyota ya utu duniani," alisema Mbatia.

"Mnaiona Tanzania, ilitumia utu kufuta machozi mama Afrika, kwa maumivu ya vita, njaa, ukame, uharibifu wa mazingira na kubwa kuliko yote janga la uongozi ndani ya Tanzania, Afrika na duniani kote wajibu wetu Watanzania kwa kushirikiana na marafiki wengine nje kuifanya dunia kuwa sehemu salama na nzuri zaidi ya kuishi sisi sote, utu ndiyo dira sahihi ya kuongoza dunia ya leo."

Pia Mbatia aliwataka Watanzania kuacha kupuuzia suala la kuchukua tahadhari za kujikinga na Uviko-19 ikiwamo kuchanjwa.

Mbatia alisema Watanzania wanatakiwa kutambua kuwa wanapochukua hatua ya kuchanja wanafanya jambo la kulinda utu kwa kuwa wanajilinda wao pamoja na wengine.

"Watanzania ambao hawajachanjwa, jamani turudishe utu wetu, tukachanjwe kwa sababu kufanya hivyo kunalinda uhai wako na wa mwingine na kuchanja ni utu," alisema Mbatia.

Alisema ni vyema kila Mtanzania atambue kuwa chanjo ni jambo la muhimu na ni vyema likazingatiwa na kila mtu ili kulinda afya zao.

"Pia, alikemea tabia za baadhi ya Watanzania wanaojenga matabaka kwa misingi ya dini, kisiasa, kiuchumi.

"Binadamu wote ni sawa hivyo kila mtu anastahili heshima na kutendewa kwa utu. Ubaguzi wa kikanda, rangi, kisiasa, kikanda ni upunguani, mtu anayebagua mwenzie kwa misingi ya imani ni upunguani," alisema Mbatia.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika alikiomba Chama cha NCCR Mageuzi kuendelea kuenzi misingi ya kuanzishwa kwake hususani kupambania uhuru wa demokrasia kwa nguvu.

"Kama ambavyo chama hiki kilianzishwa kwa misingi ya kupambania demokrasia na utu, naomba mwendeleze misingi hiyo hususani katika kupatikana kwa Katiba mpya ambayo itawezesha wakati wote mambo yanapokuwa hayaendi sawa kuyasemea," alisema Mnyika.

"Kwa mfano sasa hivi Mbowe yuko gerezani, mkawa na nguvu ya kusema aachiwe, mageuzi ni kazi ngumu, lakini kwa kweli ni maombi yangu myaendeleze kwa nguvu kubwa sana, kuyaishi kwa vitendo,

# Kampuni yataka ilipwe bil. 145/- kutekeleza amri ya mahakama

**Na Hellen Mwango**

KAMPUNI ya Coast Textiles Limited imeiomba Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kumwajibisha Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB), Richard Malisa, bodi hiyo iliyopo chini ya Benki Kuu Tanzania (BoT) ambayo ni mfilisi wa Benki ya FBME, kama haitalipa Sh. bilioni 145 ili kutekeleza hukumu ya Mahakama.

Kampuni hiyo imefungua maombi ya ikiomba utekelezaji wa hukumu iliyotolewa na Jaji Aloysius Mujulizi wa mahakama hiyo 2015 baada ya wadaiwa, ikiwamo benki hiyo ya kigeni kushindwa kuitekeleza kwa zaidi ya miaka sita.

Mlalamikaji anaiomba mahakama Sh. 145,946,500,641 zilipwe na DIB, taasisi ambayo ilichukua ufilisi wa FBME Bank na kama itashindwa, Mkurugenzi wa DIB awajibishwe kwa kulipa fedha hizo.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Naibu Msajili Crisencia Kisongo, imepanga kusikiliza maombi hayo Novemba 30, mwaka huu.

Awali, katika uamuzi uliotolewa na Jaji Joaquine De-Mello Aprili 13, mwaka huu, kufuatia kusikilizwa bila kupingwa na upande wa walalamikiwa, mahakama hiyo iliamuru DIB kulipa fedha hizo mara moja.

Hata hivyo, Wakili Joseph Rutabingwa, aliandika barua kuifahamisha DIB kuhusu uamuzi wa mahakama, lakini hakukuwa na majibu ya kutekeleza malipo husika hadi siku ya uamuzi kama ilivyoamriwa.

Hatua hiyo inakuja siku chache baada ya mamlaka ya serikali na Bunge kuelezea wasiwasi wao juu ya mamlaka mbalimbali kutotekeleza hukumu zinazotolewa na mahakama.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameishauri mahakama ianzishe utaratibu wa kuhakikisha maamuzi yanayotolewa yanatekelezwa.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa kampuni hiyo imekuwa mahakamani tangu 1997, ambayo ni miaka 24, ikitafuta haki zake dhidi ya Benki ya FBME, ambayo baadaye ilichukuliwa na BoT ili kulinda wateja wa kitanzania baada ya kuhusishwa na makosa ya utakatishaji fedha nchini Cyprus.

Mahakama Kuu ilitoa hukumu katika kesi hiyo Julai 27, 2015, ambayo ni zaidi ya miaka sita, lakini amri hiyo haijatekelezwa hadi sasa. Mkurugenzi Mtendaji wa Coast Textiles Limited, Sudhir Lakhanpal, aliwahi kuomba Ubalozi wa India kuingilia suala hilo.

Hata hivyo, juhudi hizo hazikuzaa matunda, hatua iliyomlazimu mfanyabiashara huyo kuwasilisha maombi ya kukazia hukumu iliyotolewa. Benki Kuu iliwahi kuahidi kulipa kiasi hicho cha fedha baada ya kuchukua usimamizi wa Benki ya FBME na baada ya mashauri yaliyopo mahakamani kumalizika.

Kwa mujibu wa maombi yaliyowasilishwa na Wakili Joseph Rutabingwa, kwa niaba ya kampuni hiyo, hakuna shauri lolote lililipo mahakamani linalohusu sakata la malipo hayo kufuatia kufutwa kwa majaribio kadhaa ya Benki Kuu kupinga utekelezaji wa hukumu hiyo.

Coast Textiles Limited wakati wote walikuwa wateja wa FBME Bank Limited tangu 1997 na walipatiwa mkopo na Benki ya Trust (Trust Bank), kupitia tawi lake nchini Kenya. Lakini kiasi kilichohusika, ambacho ni karibu Dola za Kimarekani 600,000, hakikuingizwa kwenye akaunti ya Coast Textiles Limited nchini India.

Mgogoro ulizuka kuhusiana na ulipaji wa mkopo huo na kusababisha FBME Bank Limited kuunganisha mikopo miwili iliyokuwa imetolewa. Coast Textiles Limited ilidai kuwa kuunganishwa kwa mikopo hiyo iliyotolewa na benki mbili ilikuwa sio sahihi na ilikiuka makubaliano.

Kwa hati ya uhamisho kutoka Benki ya Delphis (T) Limited, mtangulizi kwa jina la FBME Bank Limited, riba ya benki kutokana na mkopo uliotolewa Coast Textiles Limited ilihamishiwa kwenye Dhamana ya Utambuzi wa Mkopo na Maendeleo, mtangulizi kwa jina la kampuni ya Consolidated Holding Corporation.

Kufuatia hali hiyo, Consolidated Holding Corporation, kwa kutumia mamlaka iliyopewa kisheria, ilihamisha mali mbalimbali, ikiwamo kiwanda na mashine za Coast Textiles Limited zilizowekwa kama dhamana kwenye Benki ya FBME kupata mkopo huo ambavyo viliuzwa kwa kampuni ya Middle East Properties Limited.

Kampuni hiyo ya Middle East Properties Limited baadaye ilihamisha mali iliyopo kwenye kiwanja namba 3 LOT 20, Barabara ya Nyerere (Pugu) kwenda kampuni ya Empire Properties Limited na baadaye Five Star Investments Limited, jambo lililopekea kampuni ya Coast Textiles Limited kupeleka mgogoro huo mahakamani.

Mapema Desemba 31, 2015, mahakama ilitoa amri ya kumtaka Gavana wa BoT kukamata akaunti za Benki ya FBME ili kutekeleza hukumu lililotolewa na Jaji Mujulizi kwa ajili ya malipo hayo.

HABARI KITAIFA

## H/shauri zatakiwa kudhibiti kelele nyumba za starehe

**Na Munir Shemweta,** WANMM GEITA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Hamad Chande, amezitaka halmashauri nchini kuhakikisha zinadhibiti nyumba za starehe zinazopiga muziki wa kelele katika maeneo ya makazi ya watu.

Alisema, kuna baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya makazi, lakini ghafla maeneo hayo yanatumiwa kwa shughuli zisizopangwa kama vile kumbi za starehe na kuleta usumbufu wa kelele kwa wananchi.

"Katika halmashauri kuna maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya makazi na shughuli nyingine, lakini ghafla maeneo hayo yanabadilika na kuwa kumbi za starehe zinazopiga muziki unaoleta kelele na kukera watu, huu muhali (aibu) tuiondoe," alisema Chande.

Kwa mujibu wa Chande, halmashauri nchini zinatakiwa kusimamia mipango yake kwa kuhakikisha shughuli zinazofanyika katika maeneo yake ni zile zilizopangwa kwa kuwa mara kadhaa kumekuwa na malalamiko kuhusu mwingiliano wa nyumba za makazi na kumbi za starehe.

Waziri Chande ambaye alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kikao kati ya Kamati ya Mawaziri 8 wa Wizara za Kisekta na viongozi wa mkoa wa Geita, alisema, nyumba za starehe zinazopiga kelele za muziki kwenye maeneo ya makazi zimekuwa zikileta athari ikiwamo kwa wagonjwa wa moyo na kuzua malalamiko miongoni mwa wananchi ambapo alizitaka halmashauri zote nchini kutofumbia macho suala hilo.

Alisisitiza kwa kusema kuwa kama nyumba imepangiwa matumizi ya makazi basi itumike kwa suala hilo na si vinginevyo na kubainisha kuwa, halmashauri zihakikishe zinaandaa na kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo yake.

Kuhusu suala la usimamizi wa mazingira nchini, Chande alisema, mazingira ndiyo maisha na uhai wa binadamu na viumbe vingine, hivyo wananchi wanatakiwa kuhakikisha wanayatunza ili kuepuka kukosa rasilimali hewa.

"Ukikosa rasilimali hewa uhai na thamani ya ubinadamu imeisha na bila mazingira hakuna mifugo wala maji, mazingira yetu ndiyo maisha na uhai wetu," alisema Chande.

Awali mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri 8 wa Wizara za Kisekta katika utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 Waziri wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema, katika mkoa wa Geita imeamuliwa vijiji 37 vilivyokuwa kwenye mgogoro wa muda mrefu na maeneo ya hifadhi za misitu vibaki katika maeneo yake.

Aidha, serikali imeamua kumega sehemu ya hifadhi za misitu 9 katika mkoa wa Geita kwa ajili ya kuwapatia wananchi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hizo.

Ametaja hifadhi za misitu zilizomegwa kuwa ni Geita, Ruande, Rwamgasa, Usindakwe na Miyenze zilizoko wilayani Geita, Hifadhi ya Mbogwe iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Biharamulo-Chato pamoja na Hifadhi ya Misitu ya Runzewe na Ushirombo zilizopo Wilaya ya Bukombe.

# Vijiji zaidi ya 5,000 vyapata mawasiliano ya simu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Halotel kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (USCAF) wamefanikiwa kufikisha mawasiliano katika vijiji 5,100 ambavyo havikuwa na mawasiliano.

Pia kampuni hiyo inadhamiria kufikia idadi ya wateja milioni 10 ifikapo mwaka 2023 na kuongeza wateja wa Halopesa hadi milioni tano.

"Vile vile tunaendelea kufikisha mawasiliano sehemu ambazo bado zina changamoto ya mawasiliano ili kuongeza ubora wa huduma na kupanua wigo wa mtandao wetu katika maeneo ambayo mawasiliano yake ni duni," alisema Mkurugenzi wa Miundombinu na Ufundi, Justus Kashashari.

Mkurugenzi wa Biashara, Kampuni hiyo, Abdallah Salum, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka sita tangu ianze kutoa huduma za mawasiliano nchini mwaka 2015.

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), hadi kufikia robo tatu ya mwaka 2021 kampuni imesajili wateja milioni saba.

Aliwashukuru wateja wa Halotel kwa kuendelea kuunga mkono na kuchagua mtandao wa kampuni hiyo ambayo ina mipango madhubuti ya kuendelea kutoa huduma bora kwa wateja wake.

"Mpango wetu mwingine ni kuwekeza zaidi katika kutoa huduma ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ili kuwafanya watumiaji wa simu janja kuperuzi kwenye mitandao ipasavyo na kunufaika kutokana na mahitaji yao mbalimbali katika kuwapa maendeleo ya kiuchumi na kijamii," alisema.

Pia katika kusherehekea miaka sita imewazawadia wateja wao kupitia kampeni maalumu "Recharge promotion" mteja atapata asilimia 20 zaidi ya salio atakaloliongeza.

Pia kwa kuboresha huduma kutoka huduma ya 2G kwenda 3G na 4G kufikia lengo la kukidhi mahitaji ya mawasiliano bora katika jamii ndani ya Tanzania.

Pia kampuni imesaidia Watanzania wengi vijijini kuwa na mawasiliano bora kwa asilimia zaidi ya 80 katika vijiji vyote na kwa zaidi ya asilimia 95 nchi nzima.

"Katika miundombinu hii tumefanikiwa kutandaza nyaya za mawasiliano nchi nzima, kusimika na kutumia minara zaidi ya 4,200 Tanzania nzima inayotoa huduma kwa jamii ili kuhakikisha inafikisha mawasiliano yenye ubora zaidi na kasi kubwa katika kuperuzi na utumiaji wa mtandao," alisema.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (watatu kulia), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (wanne kulia), msaada wa mashuka na vitanda kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma. Wengine kutoka kushoto ni Mbunge wa Jimbo la Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mukunda na kulia ni Mbunge wa Jimbo la Bahi, Keneth Nolo. NMB ilikabidhi msaada wa vifaa mbalimbali yenye thamani ya Sh. milioni 180 kwa mikoa ya Simiyu, Arusha, Iringa, Rukwa, Mara, Dodoma pamoja na Kilimanjaro ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 800/- zahudumia rufani ya wagonjwa

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Medical Teams Tanzania, limetumia zaidi ya Sh. milioni 800 kwa kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka huu, kuhudumia watu katika mradi wa rufani ya wagonjwa.

Aidha, kati ya fedha hizo Sh. milioni 79 zilitumika kuhudumia wenye ugonjwa wa afya ya akili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa shirika hilo, Dk. George Mwita, wakati wa kuadhimisha Siku ya Wenye Ulemavu wa Akili Duniani, iliyofanyika mkoani Kigoma, wanaungana na wadau wote kuadhimisha siku hiyo chini ya kauli mbiu ya 'Afya ya Akili katika ulimwengu usio na usawa'.

Alisema pamoja na huduma za matibabu, shirika hilo lilitoa uangalizi wa karibu kwa wagonjwa wa afya ya akili wasio na ndugu/familia, misaada mbalimbali ikiwamo dawa, chakula, mavazi, malazi, na mahitaji mengine muhimu na msingi.

"Shirika la Medical Teams Tanzania, tunaishukuru Wizara ya Afya na serikali ya Mkoa wa Kigoma, kwa kutupa ushirikiano na kuhakikisha afya ya akili inatiliwa mkazo na wagonjwa wanahudumiwa vizuri.

"Napenda kutambua serikali ya watu wa Marekani, kwa ufadhili wa programu hii (BPRM), yenye kuleta matumaini kwa wagonjwa wa afya ya akili, ambao huduma hii ni muhimu sana kwao, kutokea Januari hadi Septemba tumeweza kuhudumia rufani za wagonjwa wa afya ya akili zaidi ya 35, ambao hukaa hospitalini kwa muda wa mwezi mmoja hadi mitatu au hata zaidi," alisema Mwita.

Aliongeza kuwa siku hiyo imekuja wakati maisha ya watu ya kila siku yakiendelea kubadilika kutokana na janga la UVIKO-19, huku kukiwa na changamoto nyingi kwa wahudumu wa afya.

Aidha, alibainisha kuwa moja ya changamoto wanazopitia wahudumu wa afya ni kutoa huduma katika mazingira magumu, pia kwa upande wa wafanyakazi, ambao maisha yao yanatishiwa, kwa ajili ya ukosefu wa ajira na fursa za kibiashara.

Kwa upande wa watu walio na ugonjwa wa afya ya akili alisema hali ni tete zaidi maana wengi wao hupata kutengwa na jamii inayowazunguka, kuliko ilivyokuwa hapo awali.

"Katika mazingira haya inatarajiwa kwamba hitaji la afya ya akili na msaada wa kisaikolojia litaongezeka sana katika miezi na miaka ijayo, pia kwa niaba ya shirika tunaomba serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan na wadau wote kwenye sekta ya afya kuongeza uwekezaji katika mipango ya afya ya akili katika viwango vya mikoani na kitaifa," alisema Dk. Mwita.

# Wakulima wataka ushiriki wadau ngazi ya chini mipango tabianchi

**Na Getrude Mbago**

WAKULIMA wa mazao na jumuiya za wazalishaji wa miti nchini wameiomba serikali kuhakikisha kuwa maandalizi ya mipango na mikakati ya mabadiliko ya tabianchi inashirikisha kwa karibu wadau na viongozi katika ngazi za chini.

Lengo ni kuharakisha juhudi zinazolenga kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zinaathiri sana jamii.

Wadau hao walitoa wito huo mjini Iringa wakati wa ufunguzi wa warsha iliyotenga kujadili changamoto za mabadiliko ya tabianchi na kuja mkakati utakaosaidia kudhabiti changamoto zitokanazo na mabadiliko hayo.

Warsha hiyo iliandaliwa na Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Uoto wa Asili (IUCN). Kikao hicho pia ni sehemu ya mradi wa Kituo cha Misitu na Shamba (FFF) ambao unasaidia jumuiya za wakulima wa mazao na miti katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Kaskazini, Kusini na Magharibi mwa Tanzania. Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) la Umoja wa Mataifa ndio mtakelezaji wa mradi huo wa FFF kwa kushirikiana na mashirika mengine na washirika wa msaada wa kiufundi kama IUCN.

Doyi Mazenzele, Ofisa Programu wa IUCN, alisema kupambana na mabadiliko ya tabianchi kunahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa wadau wote katika nyanja tofauti wakiwamo wale wa ngazi za chini za vijiji.

Alisema ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026), serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi pamoja na wasomi, utafiti na vyombo vya habari wana jukumu kubwa la kutimiza malengo ya mkakati.

Alisema kuwa mkakati huo unataka wizara za kisekta na mamlaka za serikali za mitaa kujumuisha mabadiliko ya hali ya tabianchi katika mipango na bajeti na kuweka kipaumbele katika miradi.

Ripoti zinaonyesha kuwa mabadiliko ya hali ya tabianchi kwa sasa yanaathiri sana delta za kilimo, mifugo, misitu na ufugaji nyuki, vyanzo vya maji, mazingira ya pwani na baharini - sekta ambazo zinasaidia zaidi ya asilimia 80 ya idadi ya watu wa Tanzania na ndio zinachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi.

Revocatus Njau, mwenyekiti wa Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu (MJUMITA), alisema kilimo cha kuhamahama kinachangia kwa kiasi kikubwa kumaliza miti na kuharibu uoto.

Aliiomba serikali na wadau kuwekeza katika kuwaelimisha wakulima juu ya kilimo bora kinachotunza mazingira.

Aliongeza kuwa shughuli nyingi za kibinadamu ambazo zinaharibu mazingira zinafanywa kwa sababu watu wengi hufikiria faida ya muda mfupi na wanakosa njia mbadala ya kujitafutia riziki.

Njau pia alisema kuwa viongozi wa serikali za mitaa haswa katika maeneo ya vijijini wanapaswa kuhamasishwa juu ya umuhimu wa kusimamia utunzaji wa mazingira kwani wengi wao wamekuwa wakidhoofisha miradi ya upandaji miti.

Lukas Payovela, mwenyekiti wa kikundi cha upandaji miti cha Ukombozi mkoani Njombe, alisema watoto wa shule wanapaswa kufundishwa na kuwa wadau wakubwa wa masuala ya uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kupitia mitaala.

Eva Msella, Ofisa Miradi kutoka IUCN, alinukuu vyanzo vyote vya kitaifa na kimataifa akisema kuwa kilimo kisicho endelevu, ukataji miti, mabadiliko ya matumizi ya ardhi na shughuli za viwandani ndizo sababu kuu zinazochochea kuongezeka kwa gesi chafu angani.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga (katikati), akiongea katika hafla ya kupokea msaada wa chakula kwa ajili ya wanafunzi walioko katika mwaka wa Mtihani wa Taifa Kata ya Bugarama, uliotolewa na Barrick Bulyanhulu ili kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka ufugaji kibiashara

**Na Munir Shemweta,** SERENGETI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameitaka jamii ya wafugaji wilayani Serengeti mkoani Mara kuachana na utaratibu wa zamani wa ufugaji wa kuhamahama na mifugo na badala yake waendeshe ufugaji wa kisasa uliojikita kibiashara.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Bisarara katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti mkoani Mara wakati wa ziara ya mawaziri wanane wa wizara za kisekta kuhusu utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 mwishoni mwa wiki, Ndaki alisema kwa sasa upungufu wa ardhi ya kuchungia mifugo ni mkubwa kwa kuwa idadi ya watu na mifugo kuongezeka, lakini ardhi haiongezeki.

Alisema, kutokana na hali hiyo, kuna haja kwa jamii ya wafugaji nchini kuanza kubadilika kwa kuacha kuendelea na utaratibu wa zamani wa kuhama na mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine ulioonekana kuzua migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

"Katavi, Rukwa, Mbeya, Lindi mpaka Mtwara wafugaji wamejaa na malisho haayatoshi, hivyo tusipofanya ufugaji wa kuvuna mifugo yetu tutaifugia wapi," alisema Ndaki.

Kwa mujibu wa Waziri Ndaki, ni vyema kuanzia sasa wafugaji wakàangalia namna bora ya kubadilika kwa kufanya ufugaji wa kuvuna alioueleza kuwa utawezesha jamii hiyo ya wafugaji kutumia sehemu ya fedha kwa shughuli za maendeleo.

Kwa upande wake Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri hao, aliwaeleza wananchi wa kijiji cha Bisarara wilayani Serengeti mkoa wa Mara kuwa, ni vizuri maeneo ya vijiji yaliyorasimishwa kutoka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kupangiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi utakaoainisha maeneo ya kufugia na kulima ili kuepuka migogoro ya ardhi.

Hata hivyo, Waziri Lukuvi alisemawakazi wa vijiji vilivyobakishwa kwenye maeneo ya Hifadhi ya Serengeti kuhakikisha shughuli zinazofanyika pembezoni mwa mipaka ya hifadhi kuwa za ufugaji badala ya kilimo ili kuepuka uharibu unaoweza kufanywa na wanyama.

Mbunge wa Serengeti, Dk. Amsabi Mrimi, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wa kuwajali wananchi wa vijiji kwa kuwapatia sehemu ya ardhi ya hifadhi na kueleza kuwa mtu anayetoa ardhi kwa wananchi anakuwa amewasaidia sana kwa kuwa ardhi ndiyo kila kitu.

Aliishauri serikali kupitia upya sheria ya kuhamisha mifugo kwenye maeneo ya vijiji vilivyopo kando ya hifadhi kwa kueleza kwamba sheria hiyo imeleta madhara makubwa kwa jamii ya wafugaji.

## 2 wazoa pikipiki za 'Bonge la Mpango'

**Na Mwandishi Wetu**

Wakazi wa wili wa Dar es Salaama na Morogoro wameibuka na ushindi wa pikipiki katika droo ya kwanza ya awamu ya pili ya Kampeni ya Weka Akiba na Ushinde.

Washindi hao wa kampeni inayoendeshwa na Benki ya NMB 'NMB Bonge la Mpango - 2merudi tena,' iliyofanyika jijini Dar es Salaam, ni Nakaunda Baraka Mangosongo na Charles Elias Mkwizu wakiibuka washindi wa pikipiki mbili za miguu mitatu aina ya Sky Mark.

NMB Bonge la Mpango ni kampeni itakayoendeshwa kwa kipindi cha wiki 12, ikilenga kuhamasisha utamaduni chanya wa kujiwekea akiba, ambako washindi 50 watajinyakulia pikipiki za mizigo 50 zenye thamani ya Sh. 225M, huku washindi 120 wakitarajia kujishindia fedha taslimu Sh. milioni 12.

Akizungumza kabla ya kuchezeshwa kwa droo hiyo, Meneja Mwandamizi wa Idara ya Wateja Binafsi wa NMB, Ally Ngingite, alisema katika kipindi chote cha kampeni hiyo, zawadi zote zenye thamani ya jumla ya Sh. m237, zitaenda kwa washindi 170, ambao wataweka akiba katika akaunti ama kufungua akaunti mpya zenye akiba isiyopungua Sh. 100,000.

"Kila wiki tutakuwa na droo za kupata washindi 12, wakiwemo 10 wa pesa taslimu Sh. 100,0000 kila mmoja, huku wengine wawili wakijishindia pikipiki za miguu mitatu (moja kwa kila mmoja), aina ya Sky Mark yenye thamani ya Sh. milioni 4.5.

"Wito wetu kwa wateja wa NMB ni kuendelea kujiwekea akiba ili kujiongezea nafasi ya kushinda pesa taslimu ama pikipiki.

Na kwa wale wasio na akaunti, watembelee matawi yetu yaliyotapakaa kote nchini, waweze kufungua akaunti na kuweka akiba angalau ya shilingi laki moja, waingie kwenye droo hizi na kushinda," alisema Ngingite.

Droo hiyo ilichezeshwa mbele ya ofisa toka Bodi ya Michezo ya kubahatisha Tanzania (GBT), Joram Mtafya, ambaye aliwahakikishia Watanzania na wateja wa NMB, kuwa kampeni hiyo itafanyika kwa kufuata sheria na kanuni zinazosimamia michezo hiyo na kwamba, hata akaunti za watoto walio chini ya umri wa miaka 18 (zinazoendeshwa na wazazi ama walezi), zinaweza kushinda zawadi hizo.

Ukiondoa Mangosongo na Mkwizu wa Dodoma waliojishindia pikipiki za Sky Mark, washindi wengine 10 waliojinyakulia pesa taslimu ni: Kuluthum Chande, George Fabiano, Justine Yona, Justina Mbuya na Beatrice Tarimo.

Wengine ni Gloriana Nicholaus, Paschal Phabian, Alphonce Donatus, Ramadhani Khalfan, Kelvin Mosha. Droo ya pili ya NMB Bonge la Mpango itafanyika wiki hii kupata washindi wengine 12, wakiwemo 10 wa pesa taslimu na wawili wa pikipiki.

Nipashe
Spotika



WAMILIKI 10 WA KLABU WENYE UTAJIRI MKUBWA ZAIDI 2021 UK. 12




Salah

# WASHAMBULIAJI MASHOTO WA5 TISHIO ZAIDI DIMBANI

**LONDON, England**

TULIONA Lionel Messi akifunga bao zuri dhidi ya Manchester City kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mguu wake wa kushoto. Bao lililofungwa na raia huyo wa Argentina halikuwa rahisi na bado lilikuwa la kupendeza. Daima kuna umaridadi na darasa juu ya wachezaji waanaotumia miguu ya kushoto na Messi ndiye zao bora zaidi kwa hilo.

Baadhi ya wachezaji bora kwenye mchezo huo ambao wameupamba kwa mguu wa kushoto ni Diego Maradona, Arjen Robben, Raul, Robin van Persie na wengine wengi.

Kwa ubora wa wachezaji wa kushambulia uwanjani, mchezo umekuwa wa burudani zaidi kwa miaka sasa. Kwenye makala haya, tunaangalia washambuliaji bora zaidi wanaotumia mguu wa kushoto kwa sasa, pata fursa ya kuwafahamu hapa...

**#5. Angel Di Maria (Paris Saint-Germain)**

Angel Di Maria alihitimu kutoka akademi ya kukuza soka ya Rosario Central. Wakati akiwa na klabu hiyo ya Argentina, Arsenal walitaka kumsajili, lakini ilishindikana.

Winga huyo aliishia kusaini Benfica mwaka 2007. Kutokana na kiwango bora alichokionyesha na klabu hiyo ya Ureno, Di Maria alizivutia klabu kadhaa za Ulaya. Lakini ni Real Madrid ambao waliweza kupata saini yake kwani walimsajili mwaka 2010.

Di Maria kwa ustadi wake, wepesi, uwezo wa kupiga chenga alikuwa mmoja wa washambuliaji wa kutisha pale mbele. Katika misimu yake minne na 'Los Blancos' hao, alifunga mara 22 na kusajili asisti 50 kwenye LaLiga.

Ilishangaza wakati Madrid ilipomruhusu ajiunge na Manchester United mwaka 2014, hata hivyo, Di Maria aliondoka baada ya kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Akiwa kule kwa 'Mashetani Wekundu', mchezaji huyo alikuwa na wakati mbaya zaidi ambao hatausahau. Hakuwahi kuwa na kiwango cha kuvutia na uhusiano wake na kocha wa United wa wakati huo, Louis van Gaal ulimweka kwenye wakati mbaya zaidi.

Hatimaye, Di Maria aliachana na Ligi Kuu England baada ya msimu mmoja na akajiunga na Paris Saint-Germain. Usajili wa mchezaji huyo umekuwa na faida kwa klabu hiyo ya Ufaransa. Kwenye Ligue 1, Di Maria amechangia mabao 121 huku akicheza mechi 176.

Kuwasili kwa Lionel Messi, raia hao wawili wa Argentina watatarajia kuisaidia PSG kushinda taji lao la kwanza kabisa la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. Di Maria bado ni mmoja wa wachezaji wachache ambao wamepata nafasi ya kucheza pamoja na Cristiano Ronaldo na Messi.

**#4. Romelu Lukaku (Chelsea)**

Baada ya kuhitimu akademi ya soka ya Anderlecht, Romelu Lukaku alijiunga na Chelsea katika msimu wa majira ya joto wa 2011. Kwa bahati mbaya, mshambuliaji huyo wa Ubelgiji alishindwa kupata wakati wa kucheza mara kwa mara na klabu hiyo ya Jiji la London na kwa hivyo alipelekwa kwa mkopo kwenye klabu nyingi.

Mshambuliaji huyo mwenye nguvu na mrefu alipelekwa kwa mkopo West Bromwich Albion na Everton kwenye Ligi Kuu. Baada ya kuvutiwa na kiwango chake, Everton ilimsajili kwa mkataba wa kudumu. Katika misimu yake minne na klabu hiyo ya Merseyside, Mbelgiji huyo alifunga mabao 68 na asisti 24 kwenye Ligi Kuu.

Manchester United walikuwa wakihitaji mshambuliaji na wakaishia kumsajili Lukaku. Katika mechi zake 66 za Ligi Kuu alifunga mara 28.

Lukaku alihisi alifanywa mbuzi wa kafara kule Man United kabla ya kuuzwa Inter Milan mwaka 2019. Alikuwa na wakati mzuri na klabu hiyo ya Italia, akifunga mabao 64 katika mashindano yote kwa misimu miwili. Lukaku pia aliinua taji la Serie A na Inter msimu wa 2020-21 na msimu huu wa majira ya joto akarejea Chelsea.

**#3. Erling Haaland (Borussia Dortmund)**

Erling Haaland ni kipaji cha aina yake, ni mshambuliaji wa Norway na mmoja wa wachezaji bora zaidi kwa sasa. Kuanzia maisha yake ya mpira wa miguu na Bryne kule Norway, Haaland alikuwa na ujuzi wa kufunga mabao tangu utoto. Alisajiliwa Molde mwaka 2017 na kucheza chini ya Ole Gunnar Solskjaer. Kwa uwezo wake wa kufunga mabao, ilikuwa ni suala la muda tu kabla ya mshambuliaji huyo mchanga kuwaniwa na klabu kubwa Ulaya.

Haaland alisaini Red Bull Salzburg mwaka 2019 ambapo alifunga mabao 17 na kutoa asisti nne katika mechi 16 tu kwenye Ligi ya Austria. Kwa rekodi kama hiyo, Borussia Dortmund walipendezwa naye na wakamsajili mwaka 2020.

Tangu ajiunge nao, Haaland mwenye umri wa miaka 21 hajageuka nyuma. Kwa mwili wake wenye nguvu, kasi ya kushangaza, nafasi nzuri na uwezo mzuri wa kufunga mabao, imekuwa ngumu sana kwa wapinzani kumdhibiti. Kufikia sasa, amefunga mabao 47 na kusajili asisti 15 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, katika mechi 48.

**#2. Mohamed Salah (Liverpool)**

Mshambuliaji huyo wa Misri amekuwa mchezaji nyota kwenye Ligi Kuu England kwa muda sasa. Salah aliwahi kuwa mchezaji wa Chelsea wakati alipojiunga na klabu hiyo ya London mwaka 2014. Baada ya kukosa kupata nafasi za kucheza mara kwa mara, Mmisri huyo alipelekwa kwa mkopo Fiorentina na baadaye AS Roma.

Alikuwa na wakati mzuri akiwa anacheza kwa mkopo kule Roma, baada ya hapo alisajiliwa kwa mkataba wa kudumu na akafunga mabao 34 na asisti 22 kwenye mashindano yote.

Na Liverpool wakamsajili na tangu mwaka 2017 amekuwa na 'Wekundu' hao wa Anfield.

Amekuwa na Liverpool kwa zaidi ya misimu minne sasa na amepata mafanikio mengi. Alikuwa nguzo muhimu kuisaidia Liverpool kushinda taji la Ligi Kuu msimu wa 2019-20, Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19, Klabu Bingwa ya Dunia na UEFA Super Cup.

**#1. Lionel Messi (Paris Saint-Germain)**

Hakuna mjadala linapokuja suala la ubora wa mguu wa kushoto wa Lionel Messi.

Baada ya kuhitimu kwenye akademi ya kukuza soka la vijapa pale La Masia, raia huyo wa Argentina alicheza mechi yake ya kwanza kwa Barcelona mwaka 2003. Tangu hapo hajaangalia nyuma ameendelea kuvunja rekodi nyingi, akiweka historia yake mwenyewe katika klabu hiyo.

Baada ya kukaa misimu 17 na klabu hiyo ya Catalunya, akifunga mabao 474 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga katika mechi 520. Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alishinda mataji 10 ya LaLiga, saba ya Kombe la Mfalme (Copa del Rey) na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Barcelona.

Na mpira ukiwa miguuni mwa Messi, kila kitu kinawezekana. Messi aliushtua ulimwengu wa soka msimu huu wa majira ya joto wakati alipoamua kujiunga na Paris Saint-Germain.

## ISIKUPITE

BEKI wa Kati wa Simba, Henoc Inonga Baka 'Varane' ambaye alikuwa akiitumikia DC Motema Pembe ya kwao, amechaguliwa kuwa Beki Bora wa Ligi Kuu ya DR Congo kwa msimu uliomalizika wa 2020/21, huku aliyekuwa Kocha wa AS Vita (kwa sasa RS Berkane ya Morocco), Florent Ibenge, akitangazwa kuwa kocha bora wa msimu huo.





Mmiliki wa Newcastle United, Prince Mohammed Bin Salman.

# WAMILIKI 10 WA KLABU WENYE UTAJIRI MKUBWA ZAIDI 2021

**LONDON, England**

BAADA ya miezi kadhaa ya uvumi hatimaye matajiri wa Saudi Arabia wakainunua rasmi Newcastle United.

Muunganiko wa kampuni tatu katika umiliki wa pamoja ukiwamo Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (PIF), Kampuni ya Capital Partner na RB Sports na Media.

Kulikuwa na utata mwingi wa ushiriki wa PIF katika ununuzi, lakini muungano huo uliweza kufanikiwa kuonyesha kuwa Saudi Arabia haitakuwa na udhibiti wa klabu na kwa hivyo waliweza kufaulu mtihani wa kuipata klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

Pamoja na kukamilika kwa kuichukua, Newcastle United imekuwa moja ya klabu mpira wa miguu tajiri zaidi.

Hapa tunaangalia wamiliki 10 matajiri zaidi duniani ambao wanamiliki klabu za mipira wa miguu, tendwe sasa...

#10. Guo Guangchang (Wolverhampton Wanderers) - Pauni Bilioni 5.2

Guo Guangchang, Mwenyekiti wa Kampuni ya Fosun Group, ndiye mmiliki tajiri zaidi wa 10 katika mpira wa miguu ukiwa wa thamani ya bilioni 5.2.

Kutoka mkoa wa Zhejiang Mashariki mwa China, Guangchang amekuwa mwenyekiti wa kampuni hiyo tangu mwaka 1994. Amejikita zaidi Shanghai na Hong Kong na hapo awali alifanya kazi kwenye utafiti wa masoko na baadaye akaanzisha kampuni ya Fosun Group.

Waliinunua Wolverhampton Wanderers kutoka kwa mmiliki wa zamani, Steve Morgan mwaka 2016 kwa karibu pauni milioni 45. Waliibadilisha haraka klabu hiyo kutoka ligi ya chini hadi wababe wa Ligi Kuu katika kipindi cha miaka mitano.

**#9. Zhang Jindong (Inter Milan) - Pauni Bilioni 6.2**

Licha ya matatizo ya kifedha ya hivi karibuni pale Inter Milan, upande wa Serie A una moja ya wamiliki tajiri zaidi duniani.

Zhang Jindong, mwenye umri wa miaka 58, ndiye mwanzilishi na mshika dau mkubwa wa Kampuni ya Suning na alinunua hisa nyingi katika miamba hao wa Italia kupitia kampuni yake binafsi Juni, 2016.

Wamiliki hao walianza kuwekeza sana kwenye kikosi na walimteua Antonio Conte mwaka 2019 na pia wakaimarisha kikosi cha kuwasajili kwa dau kubwa wachezaji kama Romelu Lukaku na Alexis Sanchez.

Na mwishoni walipata matunda mazuri ya uwekezaji wao baada ya 'Nerrazurri' kumaliza kusubiri kwa kipindi cha miaka 11 na kutwaa taji la Serie A katika msimu wa 2020-21.

Lakini Klabu hiyo ilijikuta katika matatizo ya kifedha msimu huu wa majira ya joto ambapo Conte aliachana nao, huku wachezaji kama Lukaku na Achraf Hakimi pia wakiuzwa.

**#8. Stan Kroenke (Arsenal) - Pauni Bilioni 6.8**

Arsenal ni moja tu ya timu nyingi za michezo duniani zinazomilikiwa na Mmarekani Stan Kroenke, pamoja na LA Galaxy Rams, Denver Nuggets na Colorado Rapids.

Kroenke alimuoa Ann Walton, mrithi wa 'Supermarket' kubwa zaidi ya Walmart ya nchini Marekani, mwaka 1974 na miaka tisa tu baadaye walianzisha kampuni ya umiliki wa mali zisizohamishika na baadaye wakaanzisha Kampuni ya Kroenke Group.

Kroenke kwa mara ya kwanza alinunua hisa kule Arsenal mwaka 2008, kabla ya kuongeza kiwango chake hadi asilimia 62 mwaka 2011.

Ukosefu wake wa uwekezaji katika klabu umewafanya washindwe kushindana kileleni mwa Ligi Kuu katika miaka ya hivi karibuni. Hata hivyo, alitumia pauni milioni 150 katika uhamisho wa wachezaji katika kipindi cha majira ya joto, na kuifanya Arsenal kuwa moja ya timu iliyofanya matumizi makubwa zaidi ya kifedha.

**#7. Philip Anschutz (LA Galaxy) - Pauni Bilioni 8.1**

Philip Anschutz alijitosa kwenye michezo baada ya hapo awali kushiriki katika biashara ya familia ya kuchimba mafuta.

Bilionea huyo mwenye umri wa miaka 81, alikuwa mmoja wa wanachama waanzilishi wa Ligi Kuu ya Marekani (MLS), na alimiliki klabu kadhaa. Hii ni pamoja na Los Angeles Galaxy, Chicago Fire, Colorado Rapids, Houston Dynamo, San Jose Earthquakes na DC United.

Anschutz baadaye aliuza hisa zake zote za klabu zake nyingine huku akibakiwa kuwa sehemu tu ya Los Angeles Galaxy.

LA Galaxy inabaki kuwa moja ya klabu maarufu zaidi Marekani na ilitambuliwa zaidi baada ya kumsajili David Beckham mwaka 2007. Pia wakawasajili, Zlatan Ibrahimovic na Javier Hernandez.

**#6. Roman Abramovich (Chelsea) - Pauni Bilioni 10.5**

Mmiliki wa Chelsea raia wa Urusi, Roman Abramovich alinunua klabu hiyo mwaka 2003 na mara moja akaibadilisha kuwa moja ya klabu zinazoongoza kwenye Ligi Kuu England na Ulaya.

Abramovich alipata utajiri katika miaka ya 1990, mwanzoni alikuwa akifanya biashara ya mbao, bidhaa za chakula, lakini mapato yake makubwa yalikuja katika biashara ya mafuta.

Tajiri huyo mwenye umri wa miaka 54, alitumia uchumi wa Urusi uliobadilika kupata utajiri miaka ya 1990, na mwaka 1995 alipata hisa ya kwenye moja ya kampuni kubwa zaidi ya mafuta nchini humo ya Sibneft.

Chini ya umiliki wa Abramovich, Chelsea imeshinda mataji kadhaa makubwa yakiwamo mataji matano ya Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili na mara tano FA.

**#5. Andrea Agnelli (Juventus) - Pauni Bilioni 14**

Andrea ni mtoto wa mwenyekiti wa zamani wa Juventus, Umberto, na familia yake ina historia ndefu kwenye klabu hiyo, wakiwa wanawasimamia Bianconeri hao tangu mwaka 1923.

Familia ya Agnelli ilianzisha Kampuni ya magari ya Fiat mwaka 1899 na kupata utajiri mkubwa. Familia hiyo pia inamiliki Ferrari kama sehemu ya kampuni kubwa ya Exor.

Mei 2010, Andrea aliteuliwa na binamu yake kama mwenyekiti wa bodi ya Juventus na kuwa mwanachama wa nne wa familia kuendesha klabu hiyo. Uteuzi wake uliambatana na skendo ya upangaji wa matokeo kabla ya kuwajibika na baadaye kusimamia mabadiliko ya uwanja mpya.

**#4. Dietrich Mateschitz (RB Salzburg / RB Leipzig) - Pauni Bilioni 15.7**

Safari ya Mjasiriamali wa Austria, Dietrich Mateschitz ya kuwa bilionea ni ya kuvutia sana.

Wakati wa likizo nchini Thailand, Mateschitz alipata kinywaji cha 'eneji' cha Red Bull. Kinywaji hicho tayari kilikuwa maarufu kwa wafanyakazi wa Thai baada ya kuanzishwa nchini humo miaka ya 1970 na mfanyabiashara, Chaleo Yoovidhya.

Mateschitz alikipenda sana kinywaji hicho, aliwasiliana na waanzilishi wa Kampuni ya Thai. Alikuwa tayari kuwapa sehemu ya asilimia 49 katika kampuni hiyo ikiwa wako tayari kumruhusu achukua fomula hiyo na kuipanua duniani. Walikubali pendekezo lake kwa furaha.

Aliipeleka duniani, lakini ilikuwa hadi mwaka 1997 ilipozinduliwa nchini Marekani na kuwa moja ya kinywaji kikubwa zaidi duniani.

Mateschitz aliwekeza fedha zake kwenye michezo hasa kwenye Formula One na alijitosa kwenye mpira wa miguu. Aprili 2005, aliinunua timu ya Austria Salzburg na baadaye akaibadilisha jina kuwa Red Bull Salzburg. Alianzisha pia RB Leipzig mnamo Mei 2009.

**#3. Sheikh Mansour (Manchester City) - Pauni Bilioni 23.2**

Sheikh Mansour aliinunua Manchester City Septemba, 2008 na mara moja akaibadilisha na kuwa yenye nguvu Ulaya na duniani.

Mansour ni Naibu Waziri Mkuu wa Falme za Kiarabu na anatoka katika familia ya Kifalme ya Abu Dhabi. Yeye pia ni Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Uwekezaji ya Mubadala ya Abu Dhabi na mwanachama wa bodi ya Kampuni ya mafuta ya kitaifa ya Abu Dhabi. Pia anasimamia kama Mwenyekiti wa Shirika la Nishati ya Nyuklia ya Emirates, Benki ya Biashara ya Abu Dhabi na Emirates Global Aluminium.

Tangu alipochukua Manchester City, tajiri huyo mwenye umri wa miaka 50, pia amezinunua New York City FC, Melbourne City FC na Mumbai City FC, kati ya zingine, kupitia Kampuni ya City Football Group.

**#2. Mamlaka ya Uwekezaji ya Qatar (Paris Saint-Germain) - Pauni Bilioni 220**

Ikiongozwa na Nasser al-Khelaifi, Paris Saint-Germain inamilikiwa na Mamlaka ya Uwekezaji ya Qatar, mfuko mkuu wa utajiri wa nchi.

Al-Khelaifi alipokuwa kijana alikuwa hodari zaidi katika mchezo wa tenis na alishiriki katika mashindano makubwa mara mbili ya ATP Tour. Katika mchezo wa tenis ukamleta Al-Khelaifi kuwa karibu na Emir wa Qatar, Sheikh Tamim.

Tamin, ambaye alikuwa mkuu wa mfuko mkuu wa utajiri, alimkabidhi rafiki yake wa muda mrefu Al-Khelaifi kazi kadhaa kwa miaka mingi katika kampuni zake.

Mwaka 2008, aliteuliwa kama Mwenyekiti wa Shirikisho la Tenisi la Qatar. Miaka mitatu baadaye, Al-Khelaifi alikuwa Mwenyekiti wa Uwekezaji wa Michezo wa Qatar, Kampuni Tanzu ya Mamlaka ya Uwekezaji ya Qatar. Inasemekana kuwa na thamani ya karibu pauni bilioni 220, iliundwa kutofautisha mali za nchi mbali na utajiri wa mafuta.

Kampuni hiyo iliamua kuinunua PSG mwaka 2011, na Al-Khelaifi alifanywa mara moja kuwa Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa klabu hiyo.

Tangu kuichukua, PSG ilitawala Ligi ya Ufaransa na hata soko la uhamisho wa wachezaji. Klabu ilimsajii Neymar kwa uhamisho ghali zaidi katika historia ya mpira wa miguu kwa kulipa pauni milioni 222 mwaka 2017. Pia walifanikiwa kumsajili Lionel Messi kwa uhamisho wa bure wakati wa majira ya joto yaliyopita.

**#1. Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (Newcastle United) - Pauni Bilioni 320**


Baada ya miaka 14 ya umiliki wa Mike Ashley, Newcastle United sasa inamilikiwa na mfuko wa uwekezaji wa Serikali ya Saudi Arabia na kuifanya kuwa klabu tajiri zaidi katika mpira wa miguu duniani.

Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia unawekeza kwa niaba ya serikali ya nchi hiyo.

PIF inajivunia mali yenye thamani ya pauni bilioni 320, na hisa katika kampuni zinazoanzia Softbank hadi Boeing, Facebook na Uber.

## Nukuu

"Uwezo wa kushinda tuzo ya Ballon d'Or inamaanisha mengi kwangu, inanifanya nijisikie fahari. Kama ukitazama kila kitu nilichofanikiwa, si tu mwaka huu, mwaka jana pia walipofuta sherehe za tuzo hizo, nimeshinda mataji mengi, nimefunga mabao mengi. Mafanikio yangu yanazungumza yenyewe kwa sababu miaka yangu miwili iliyopita nimekuwa na mafanikio makubwa," **Mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski kuelekea tuzo za Ballon d'Or 2021**



"Nadhani ni kombe langu la mwisho la Dunia. Ninaona kama la mwisho kwa sababu sioni nikiwa nina nguvu ya akili kuendelea na soka tena. Nitafanya kila kitu kujitoa vizuri na kushinda na nchi yangu kutambua ndoto yangu kubwa tangu nilipokuwa mdogo, natumai naweza kuifanya, **" mshambuliaji wa Brazil, Neymar.**



"Wakati kila kitu kinakwenda sawa na unatoa michango mikubwa, kama vile Frenkie [de Jong] amefanya, basi hakuna kitu cha kuhofia. Lakini wakati mambo yanapokwenda mrama, watu wa Barcelona kila wakati wanaangalia wageni, na inatumika kwa kocha [Ronald Koeman] vile vile, **" Kocha wa zamani wa Barca, Louis van Gaal akieleza 'historia inajirudia' na sasa yanamkuta Koeman**



# KADI 26 ZILIVYOTEMBEA LIGI KUU BARA YANGA IKIKWEPA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikianza Jumamosi iliyopita baada ya kusimama kwa wiki moja kupisha mechi za kimataifa zilizo kwenye Kalenda ya FIFA, timu ya Yanga haijapata kadi yoyote ile hadi kufikia raundi ya pili ya ligi hiyo.

Yanga ambayo ilicheza mechi mbili dhidi ya Kagera Sugar, ikishinda bao 1-0, pia ikipata ushindi kama huo dhidi ya Geita Gold FC, kesho inatarajia kushuka Uwanja wa Majimaji Songea kucheza mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC.

Mbali na Yanga, pia timu za Coastal Union na Mtibwa Sugar nazo zilikuwa hazijapata kadi yoyote hadi kufikia raundi ya pili kati ya timu 16 zinazoshiriki Ligi Kuu, lakini tayari zimeshacheza mechi za raundi ya tatu.

Juzi Mtibwa Sugar ilicheza dhidi ya Geita Gold na Coastal Union ikicheza jana dhidi ya Ruvu Shooting. Kwa maana hiyo ni Yanga ambayo mpaka sasa ina rekodi ya asilimia 100 kutopata kadi yoyote mpaka sasa, hadi itakapocheza mechi yake kesho.

Takwimu za Ligi Kuu zinaonyesha kuwa jumla ya kadi 26 zilikuwa zimeonyeshwa hadi kufika raundi ya pili, 24 zikiwa za njano na mbili nyekundu.

Katika makala haya tumekusanya majina ya wachezaji wote walioonyeshwa kadi, pamoja na timu zinazoongoza kuwa na kadi nyingi mpaka sasa, shuka nayo sasa...

**#1. Geita Gold - Kadi 4**

Timu ya Geita Gold ndiyo iliyoongoza kwa kuwa na kadi nyingi mpaka kufikia raundi ya pili, ikiwa na jumla ya kadi nne, ambazo zote ni za njano.

Geita Gold, ambayo imeanza kucheza Ligi Kuu msimu huu, kwa mechi mbili tu ilizocheza dhidi ya Namungo FC na kufungwa mabao 2-0 na bao 1-0 dhidi ya Yanga, inaonyesha kuwa ni timu ya 'kupiga viatu', lakini wachezaji wake kutokuwa na nidhamu ya mchezo.

Walioonyesha kadi mpaka sasa ni Hamisi Kadikilo, Yusuph Kagoma, Daniel Lyanga na Dereck Mussa.



Winga hatari wa Yanga, Jesus Moloko.

**#2. KMC - Kadi 3**

KMC inashika nafasi ya pili kwa kuonyeshwa kadi nyingi kwenye ligi hadi kwenye raundi ya pili, kwa wachezaji wake kuonyesha kadi mbili za njano na moja nyekundu.

Ismail Gambo alipigwa kadi nyekundu, huku wachezaji wenzake Hassaan Kapalata na Kenny Mwambungu nao wakilimwa njano.

**#3. Dodoma Jiji - Kadi 3**

Dodoma Jiji nayo kama ilivyo KMC, ipo kwenye nafasi ya pili kwa kuwa na kadi nyingi kwenye ligi, ikiwa na kadi mbili za njano na moja nyekundu. Ikumbukwe kuwa kadi mbili nyekundu ambazo zimetolewa mpaka sasa, timu za Dodoma Jiji na KMC ndizo zilizohusika.

Anuary Jabir alizawadiwa kadi nyekundu, Oktoba Mosi kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Uwanja wa Jamhuri Dodoma, timu yake ikicheza dhidi ya Simba. Aliipata kwa kumpiga kiwiko Kennedy Juma. Waliopata kadi za njano ni Seiof Rashid na Salmin Hoza.

**#5. Ruvu Shooting - Kadi 2**

Wachezaji wa Ruvu Shooting waliopata kadi za njano ni Mohamed Makaka na Nathaniel Chilambo. Makaka ambaye ni kipa wa timu hiyo, yeye aliipata kwa kupoteza muda kwenye mechi dhidi ya Biashara United, ikishinda bao 1-0.

**#6. Prisons - Kadi 2**

Wachezaji wa Prisons ambao wamekutana na kadi za njano ni Doto Ramadhani na Athanas Mdamu.

**#7. Mbeya City - Kadi 2**

Eliud Ambukile na Peter Mapunda ni wachezaji wa Mbeya City ambao wamezawadiwa kadi za njano hadi kufikia raundi ya pili.

**#8. Mbeya Kwanza - Kadi 2**

Ni Paul Peter na Salum Chuku ambao wana kadi za njano kila mmoja kwenye kikosi cha Mbeya Kwanza.

**#9. Simba - Kadi 1**

Meddie Kagere ndiye mchezaji pekee wa Simba aliye na kadi ya njano. Na aliipata Oktoba Mosi kwenye mechi dhidi ya Dodoma Jiji, baada ya kuvua jezi, akishangilia bao pekee alilofunga timu yake ikishinda 1-0.

**#10. Azam FC- Kadi 1**

Azam nayo mpaka sasa ina kadi moja, ambayo alipewa Nicolaus Wadada, beki namba mbili wa kikosi hicho.

**#11. Namungo - Kadi 1**

Mchezaji pekee wa Namungo FC aliyelimwa kadi ya njano ni Abdulaziz Makame, kiungo mkabaji wa timu hiyo.

**#12. Kagera Sugar - Kadi 1**

Kiungo mkabaji wa Kagera Sugar, raia wa Ghana ndiye anayeifanya Kagera Sugar kuwa na kadi ya njano moja, hadi kufikia raundi ya pili.

**#13. Polisi Tanzania - Kadi 1**

Wala haitoshangaza kuona kuwa mchezaji pekee mwenye kadi ya njano kwenye kikosi cha Polisi Tanzania ni beki wa kati, Kelvin Yondani.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah, ameifikia rekodi iliyowekwa na nguli wa zamani wa Chelsea na Ivory Coast, Didier Drogba ya kuwa Mwafrika mwenye mabao mengi zaidi (104) kwenye Ligi Kuu England.



# 'Watumishi Afya wanapuuza mwongozo usafi wa mikono'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa baadhi ya watumishi wa afya hawazingatii mwongozo wa usafi wa mikono uliotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), huku simu zao za mkononi zikitajwa kuwa hatari kutokana na kuhifadhi bakteria wa magonjwa ya kuambukiza.

Mfamasia Erick Venant, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa mada ya uelewa na unawaji mikono kwa vitendo kwa watumishi wa afya ili kujiepusha na magonjwa hayo kwenye Kongamano la Afya Tanzania (THS) ikiwa ni miongoni mwa mada saba zilizotolewa na Mradi wa HPSS-Tuimarishe Afya unaotekelezwa na Shirika la Swiss TPH kwa ufadhili wa Shirika la Ushirikiano na Maendeleo la Uswisi (SDC).

Alisema pamoja na kuwa usafi wa mikono ni njia bora ya kupunguza hatari ya maambukizi ya magonjwa, lakini baadhi ya watumishi hao hawazingatii hilo licha ya kupatiwa mafunzo na upatikanaji wa vifaa vya kunawa mikono.

Mtaalamu huyo alisema katika utafiti uliofanywa wa kutathmini maarifa, uwapo na upatikanaji wa vifaa vya usafi wa mikono na uzingatiaji wa mwongozo wa WHO, ulionyesha zaidi ya asilimia 75 ya watumishi wa afya Mkoa wa Dodoma wamepata mafunzo ya usafi wa mikono na kuwa na uwezo wa kufikia vifaa vya kunawa mikono. Hata hivyo, alisema asilimia 63 ya madaktari, wauguzi na wanafunzi walio kwenye mafunzo kazini 270 waliofanyiwa utafiti huo Mkoa wa Dodoma walibainika wanauelewa kuhusu unawaji mikono kulingana na mwongozo wa WHO huku asilimia 2.6 wamekuwa wakitekeleza kikamilifu mwongozo huo.

Alibainisha kuwa kwenye utafiti huo ulibaini asilimia 34 ya simu za watumishi zilizotumika kama sampuli kwenye utafiti huo zilikuwa zina bakteria mbalimbali kama Staphylococci, ambao wana usugu kwa dawa ya penicillin na upinzani wa tiba kwa dawa aina ya Erythromycin, Clindamycin na Gentamycin.

Alisema simu zao mkononi zina hatari ya kuwa chombo cha kuhifadhi bakteria wanaoambukiza magonjwa kutokana na kushikwa bila kunawa wakati au baada ya kutoa huduma.

"Utaratibu mdogo wa usafi wa mikono unamaanisha kuwa simu za mikononi za watumishi wa afya zinaweza kufanya kazi kama hifadhi ya vijidudu vinavyoambukiza," alisema.

Alifafanua kuwa usafi wa mikono ndiyo njia bora zaidi ya kupunguza hatari ya maambukizo yanayohusiana na huduma za afya na kuwaasa watumishi wa afya kuzingatia hilo.

"Simu za mkononi ni chanzo cha usambazaji vimelea vya uchafu zinapaswa kujumuishwa katika mafunzo ya usafi wa watumishi wa afya(HCW), mwongozo wa WHO unahimiza usafi wa mikono ikiwa ni njia ya kuzuia kuenea kwa bakteria wanaoambukiza na mipangilio ya utunzaji wa afya ambayo hufanyika zaidi kupitia mikono iliyochafuliwa ya wafanyakazi wa huduma ya afya, vitu au vifaa na mazingira," alisema.



Ofisa Mkuu wa Fedha TANESCO, Renata Ndege (katikati), akikabidhi kompyuta kwa Makamu Mkuu wa Shule ya Wasichana Kondoa, Alvin Lema (aliyevaa sharti nyeusi), pamoja na wanafunzi wa shule, TANESCO kupitia TUICO wanawake wametoa msaada wa kompyuta, vitanda, magodoro na mashuka vyenye zaidi ya Sh. milioni 23, hafla iliyofanyika jana wilayani Kondoa mkoani Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Chamwino yaweka kibano dhidi ya ndoa za utotoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na ndoa za utotoni katika Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma katika Kata ya Mpwayungu, matangazo ya ndoa za mabinti chini ya miaka 18, yamepigwa marufuku kanisani ili kuondokana na tatizo hilo.

Mtendaji wa Kata hiyo, Selemani Kibakaya, aliyasema hayo mwishoni wa wiki kwenye mkutano wa kujadili Mpango Kazi

wa Taifa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA)

ulioandaliwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Women wake up (WOWAP) na kushirikisha kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto ngazi za Kata na Vijiji vya Mpwayungu, Chikola na Nagulo wilayani humo.

Alisema kwa sasa hakuna taarifa za kuripotiwa kwa ndoa hizo kutokana na mapadri na wachungaji kukataa matangazo ya ndoa hizo.

"Ndoa za utotoni chini ya miaka 18 huwa hazitangazwi kanisani, zinapingwa katika kata, sehemu za ibada mtu kwenda kuandikisha ndoa chini ya miaka 18 hairuhusiwi," alisema.

Aidha, alisema jamii imekuwa na uelewa na imekuwa ikitoa taarifa juu ya vitendo vya ukatili ikiwamo ndoa za utotoni.

Hata hivyo, alisema umaskini unasababisha baadhi ya wazazi kufumbia macho watu waliowapa mimba mabinti zao wadogo.

"Mtoto anabakwa anapewa mimba, mzazi anapewa Sh. 200,000 fedha ambazo

hajawahi kuzishika tangu azaliwe anakubali na kesi inaishia hapo na mzazi ukimfuata anasema mtoto si wa kwangu kwani kuna shida gani

katika hali kama hiyo hawezi kutoa ushirikiano," alisema.

Naye Shekhe wa Kata hiyo, Nurdin Ndunguru, alisema kamati za MTAKUWWA zinafanya kazi kubwa ya kufuatilia ukatili unafanyika katika jamii.

"Lakini bado kuna baadhi ya watu wanatetea uhalifu, mhalifu anakuja kukusuta mtaani, kesi inakwenda polisi lakini hakuna kinachoendelea, ukatili huu unamalizwaje wakati watu wanakamatwa na hawachukuliwi sheria," alisema.

Ofisa wa Polisi, Emmanuel Maduma kutoka Kituo cha Polisi cha Mpwayungu, alisema kuna matukio ya ukatili yanayoripotiwa kama ubakaji, kuwapa mimba wanafunzi na shida iliyopo ni ushirikiano kati ya wazazi na vyombo vya dola. Alisema kati ya matukio 10 ni matukio mawili au matatu wazazi hutoa ushirikiano.

"Unaletewa kesi ya ubakaji tukio limetokea siku nne hadi tano ukiandika ripoti hata ushahidi unapotea, angewahi daktari angempima angekutana na michubuko, mbegu vingesaidia kwenye ushahidi," alisema.

# TANESCO yawaonyesha fursa wanafunzi wa kike

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO), limewataka wanafunzi wa kike kusoma kwa bidii masomo ya sayansi ili kupata mafundi wa kada mbalimbali za sekta hiyo.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa shirika hilo, Renatha Ndege, aliyasema hayo jana kwenye hafla ya kutoa msaada wa kompyuta, vitanda vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 23 kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa ambapo msaada huo umetolewa na Shirika hilo kupitia wanawake wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), tawi la Makao Makuu ya TANESCO.

Alisema wametoa msaada huo kwa shule hiyo ili kuweka hamasa kwa wanafunzi wa kike kusoma zaidi masomo ya sayansi ili kupata mafundi wa kada mbalimbali kutokana na baadhi kuyakimbia masomo hayo kwa kisingizio kuwa ni magumu jambo ambalo si la kweli.

"Tumekuja Kondoa Girls, kikubwa tumekuja kuwasalimia kuongea nao mabinti zetu, tumekuja kama wanawake wa Makao Makuu wa Tawi la TUICO tumekuja kwa niaba ya shirika zima kuwaletea misaada, kwa kuwa Shirika linatamani kuwa na mafundi wengi wanawake hivyo tumefika shule kuwahamasisha kusoma kwa bidii masomo ya sayansi," alisema.

Aliongeza: "Inawezekana, wajitahidi kwenye mchepuo wa sayansi kwa kuwa ukiangalia shirika letu tunatumia mafundi wengi. Tunatamani tuwe na wahandisi wengi katika shirika letu."

Alitoa wito kwa mashirika na taasisi zingine kuiga mfano wa shirika hilo kwa kuzisaidia shule zenye mahitaji ili kuwasaidia wanafunzi wafikie ndoto zao kielimu.

"Wito wetu kwa mashirika ama taasisi zingine ambao wana uwezo ni kwenda katika mashule kama haya kuwasaidia hawa watoto ili waweze kufikia malengo yao tukisaidiana tutawafikisha mbali katika kuhakikisha tunakuza elimu," alisema.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Shule ya Wasichana Kondoa, Alvin Lema, alishukuru kwa msaada huo na kwamba utasaidia kutatua kero zilizokuwa zikiwakabili wanafunzi hao.

"Pia, tunashukuru kwa kompyuta kwa kuwa sasa katika teknolojia vifaa hivi tutavitumia vizuri na tunaahidi hatutawaangusha na vifaa hivi vitatusaidia kuboresha matokeo yetu katika mitihani ya kitaifa tunajua hivi vifaa vitawasaidia sana kwani wataingia katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia," alisema.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa TUICO Tawi la Makao Makuu Idara ya Wanawake, Neema Mbuja, alisema wamepeleka msaada huo kutokana na shule hiyo kufanya vizuri katika mitihani yake hivyo wanajukumu la kuwasaidia watoto hao wa kike kutimiza ndoto zao.

"Kikubwa tulivutiwa kuja kutoa huu msaada kwa sababu tuliona ni watoto wenye mahitaji hivyo tuliona ni bora kuja kushirikiana nao katika kile kidogo, tumeleta msaada kwa sababu kwanza shule inafanya vizuri lakini sisi kama TUICO tunalojukumu la kuwasaidia wanawake kwa ajili ya kuhakikisha wanasimama wapende masomo ya sayansi sisi ni mama zao ni dada zao tumekuja kuwatia moyo kwamba elimu ndio msingi wa kila kitu," alisema.



# Mtafiti: Wakulima hawapendi kutumia mbolea

**Na Grace Mwakalinga,** IRINGA

WAKULIMA wengi wa Nyanda za Juu Kusini, wana mtazamo hasi na hawapendi kutumia mbolea zenye madini ya sulfur mashambani, hali inayosababisha udongo wa maeneo mengi kuwa na tindikali ambayo imepunguza tija kwenye uzalishaji wa mazao.

Hayo yalithibitishwa mwishoni mwa wiki na Mtafiti wa udongo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kituo cha Uyole, Watson Matamwa, wakati wakiwasilisha taarifa ya vipimo vya utafiti wa hali ya udongo Mkoa wa Iringa.

Alisema baadhi ya wakulima, ukanda wa Nyanda za Juu Kusini wana mitazamo hasi kuhusu matumizi ya mbolea yenye sulfur wakidai inaharibu udongo na kwamba ni uelewa mdogo wa wananchi.

"Tuna kazi kubwa ya kuwaelimisha wakulima wetu kuhusu matumizi ya mbolea hizo zenye sulfur kwa sababu zinasaidia kurutubisha afya ya udongo na kuongeza tija ya mazao shambani," alisema Mtafiti Matamwa.

Kwa upande wake Mtafiti Fredrick Mlowe, alisema ardhi ya Iringa ina kiwango cha chini cha Sulfur ambayo inasababisha mavuno mengi hususani ngano na mpunga kutokufikia tija kwa mkulima.

Alisema TARI wanaendelea kufanya utafiti wa udongo mikoa mbalimbali ya Nyanda za Juu Kusini na kubuni teknolojia ambazo zitasaidia kuongeza virutubisho kwenye ardhi na kuwasaidia wakulima kupata mavuno mengi, pia kukabiliana na magonjwa kwenye mimea.

Baada ya taarifa kuonyesha Mkoa wa Iringa unakabiliwa na tatizo la virutubisho kwenye udongo, Mkurugenzi wa TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema rutuba kwenye udongo imepungua.

Alishauri wakulima kutumia vipimo sahihi kila wanapotumia mbolea ili kutokuathiri udongo na mimea shambani.

Wafadhili wa Mradi wa upimaji wa udongo katika mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Mbeya na Iringa, Kampuni ya OCP, Profesa Mshindo Msola, alisema hatua zilizochukuliwa kukabiliana na upungufu wa virutubisho vya udongo ni kutoa elimu ya matumizi ya mbolea pamoja na usambazaji wa pembejeo hiyo ili kuwasaidia wakulima kupata mavuno mengi na kujikwamua na umaskini.

Hata hivyo, Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uchumi Mkoa wa Iringa, Wilfer Myuyu, alisema watakwenda kufanyia kazi ripoti hiyo ili kuongeza virutubisho kwenye udongo.




Mwanahabari mkongwe nchini Jenerali Ulimwengu aliyeketi (katikati), akiteta jambo na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi (SUGU), wakati wa kongomano la Miaka 25 ya Rai ya Jenerali Demokrasia na Ukuu wa Katiba Tanzania jijini Mbeya Jana. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Ulimwengu ataja umuhimu Katiba mpya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATANZANIA wamehamasishwa kupaza sauti zao kudai Katiba mpya ambayo itasaidia kukidhi mahitaji yao na kuongeza uwajibikaji baina ya viongozi na wananchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mwandishi mkongwe nchini, Jenerali Ulimwengu, wakati wa mdahalo wa kufanya uchambuzi wa Rai ya Jenerali Juzuu ya tatu iliyokuwa na mada isemayo Miaka 25 ya Rai ya Jenerali Demokrasia na Ukuu wa Katiba Tanzania uliofanyika jijini hapa.

Alisema madai ya Katiba Mpya sio matakwa ya wanasiasa bali ni ya kila mwananchi kwa umuhimu huo kila mmoja ashiriki kudai ili upatikane kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

"Mimi ni muumini wa haki ambaye kwa utashi wangu na ukongwe wangu, naamini ili tupige hatua na kuongeza uwajibikaji Katiba Mpya ni suluhisho, tushirikiane bila kujali itikadi za kisiasa, dini wala rangi kwa sababu katiba itamnufaisha kila mwananchi," alisema Ulimwengu.

Alisema maandiko mengi aliyoanza kuandika tangu enzi za Hayati Mwalimu Nyerere hadi sasa yanalenga kuhimiza utawala bora na sheria ili kila mmoja awajibike kwa nafasi yake.

Aliwaonya wananchi kuwa makini na baadhi ya wanasiasa ambao wanapohitaji madaraka hunyenyekea na kutoa zawadi na wanapopata madaraka hutoa mabawa.

Miongoni mwa washiriki wa mdahalo huo ambao uliwahusisha pia Kituo cha Haki za Binadamu nchini (LHRC), Ofisa Programu wa Kituo hicho, Tito Magoti alisema Katiba Mpya itakuja na suluhisho na kuhakikisha usalama kwa wananchi wanaotoa maoni kwa lengo la kuboresha serikali.

Alisema Katiba Mpya inafukia mashimo yote yanayoonekana sasa na itasaidia wananchi kwa kushirikiana na viongozi wao kujipatia maendeleo.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi (Sugu), alimpongeza Jenerali Ulimwengu kwa kuanzisha mdahalo huo nchini na kwamba kwa kuwa tayari mchakato wa Katiba mpya ulianza ni vyema sasa kura zikaanza kupigwa ili kuipitisha katiba hiyo.

Alisema ni fedha nyingi zilitumika katika mchakato huo ambao ulizingatia mahitaji ya wananchi na kutolewa kwa maoni kinachohitajika ni kuanza kwa utaratibu wa kupiga kura kwa wananchi ili kuipitisha ianze kutumika.

Baadhi ya wananchi akiwamo Felister Kaisi, Mkazi wa Nsalala mjini Mbalizi alisema wananchi wasiogope kupaza sauti kudai haki kwa sababu wanatimiza haki yao ya kikatiba.

Alisema baadhi ya viongozi wakipata madaraka wanajisahau na wanapokumbushwa huwa wakali na kuwadharau wananchi jambo ambalo alidai halikubaliki.

## Wanafunzi Chuo cha Kilimo watoa ombi kwa TARI

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAFUNZI wa Chuo cha Kilimo cha Mbalizi Polytechnic, wamewaomba wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole, kupima afya ya udongo chuoni hapo ili kuendelea kuzalisha miche ya mazao kwa ubora unaotakiwa na kujiingizia kipato.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Getrude Mbembati, alisema hitaji lao kwa sasa ni kupimiwa afya ya udongo chuoni hapo kwa ajili ya kuzalisha miche ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda na baadaye kuiuza kwa jamii inayowazunguka.

Alisema hadi sasa TARI -Uyole wamewapatia miche na mbegu za aina mbalimbali huku wakiwapatia elimu ya namna ya kuotesha na kuhudumia mimea hiyo.

"Tunawashukuru Kituo cha Uyole kwa kutupatia elimu kilimo bora pamoja na miche ambayo tunaendelea kuitunza hapa chuoni kwetu, jambo la muhimu kwa sasa ni kuomba wataalam kupima udongo wa hapa ili kufahamu ni aina gani ya mbegu au miche inayostahili kupandwa hapa, lakini tukibaini tatizo mtatusaidia kutengeneza afya ya udongo," alisema Mbembati.

Mkurugenzi wa TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema walibaini tatizo kubwa kwenye afya ya udongo hivyo wameanzisha mradi wa kupima udongo katika mikoa minne ikiwamo Mbeya, Rukwa na Morogoro.

Alisema wataalamu wa kituo hicho watakuwa wanapima udongo ili kujua tatizo lililopo pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao.

Mkuu wa Chuo cha Mbalizi Polytechnic College, Essau Mwasegile, alisema wamewajengea wanafunzi uwezo wa kuzalisha mbegu za aina mbalimbali na namna ya kuhudumia.

Alisema wamewajengea uwezo wa kwenda kuwafundisha wakulima namna bora ya kilimo bora pamoja na kuwapatia ushauri wanapokabiliwa na matatizo katika uzalishaji.

Mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, Gidion Malifimbo, alisema kwa sasa ana uwezo wa kutoa ushauri wa kilimo chenye tija kwa jamii yake na atakuwa mkulima wa mfano kwa kuzalisha kwa kuzingatia utaalamu.



## Wazanzibar watakiwa mwamko wa kujikatia bima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, amesema wananchi wa Zanzibar hawajawa na utamaduni wa kukata bima ambazo zinasaidia kujikinga na majanga mbalimbali.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya bima ya kiislamu (TAKAFUL) kwa viongozi wa dini yaliyofanyika mjini hapa.

Alisema mwamko wa wananchi kukata bima ya nyumba au kilimo ni mdogo na husababisha kupata hasara kubwa wanapopatwa na majanga.

Aidha, alisema wananchi wengi wa Zanzibar wamekuwa na kiu kubwa ya bima ya kiislamu ambayo inafuata misingi ya dini ya kiislamu kutokana na imani zao za dini na kuzitaka mamlaka ya bima (TIRA) kuanza kuandaa miongozo kwa mujibu wa sheria na ili kutoa fursa kwa bima hiyo ya kiislamu kuanza kutumika.

Alisema uchumi wowote unahitaji mifumo imara ya kifedha na matarajio ya serikali ni kuwa na mfumo imara wa kiuchumi ambao utasaidia kuongeza ajira, kodi na pato la taifa.

Naye Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Mussa Juma, alisema bima hiyo ipo duniani kote na imekua chanzo kikubwa cha uchumi wa nchi na mamlaka ya bima ilianza mchakato wa bima hiyo tangu mwaka 2014 ili kujiridhisha na kuweka mipango na muda mfupi itaanza kutumika.

Alisema wameanza kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kuelewa umuhimu wa bima hiyo ambayo inautofauti na bima zingine zilizo zoeleka.

# Mwanaharakati adai uteuzi Bodi ya Vileo haukuwa sawa

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAHARAKATI wa Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ali Makame Issa, amesema haikuwa muafaka serikali kuteua Bodi ya Ushauri na Udhibiti wa Vileo kimyakimya wakati ni kinyume na utaratibu wa kisheria.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mjini hapa, alisema bodi ya vileo inapaswa kutangazwa ili wananchi wapate kuwafahamu viongozi walioteuliwa katika mwonekano na maadili yao ili kupimwa jinsi ya kusimamia sheria kutokana na tatizo la vileo kuendelea kuwa kero visiwani Zanzibar.

"Tunampongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kuunda bodi ya vileo, lakini tunaombwa itangazwe rasmi kama anavyofanya Katibu Mkuu Kiongozi katika teuzi zingine zinazofanyika...lakini inatushangaza hili kufanyika kimyakimya," alisema mwanaharakati huyo.

Aidha, alisema bodi mpya inapaswa kusimamia sheria kwa sababu hivi sasa kuna wawekezaji wa kizungu katika sekta ya utalii pia wanaingiza vileo na kuikosesha mapato serikali jambo ambalo linapaswa kuangaliwa na serikali ili kulinda mapato na kutekeleza sheria ya vileo namba tisa ya mwaka 2020.

"Kuna wawekezaji wa kizungu katika sekta ya utalii pia wanaingiza pombe kutoka nje ya Zanzibar wakati sheria imesema waingizaji lazima wawe Wazanzibari wenye sifa za uzawa kwa mujibu wa Katiba na sio Wazanzibari wakaazi tunataka bodi mpya isimamie sheria kama ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi," alisema.

Alisema serikali lazima isimamie misingi ya sheria hasa katika suala la zabuni ili kuepusha mambo mengi kwenda kinyume na sheria kama ilivyojitokeza katika hoteli ya Bwawani Zanzibar.

"Hoteli ya Bwawani imevunjwa kwa kupewa mwekezaji, lakini hadi sasa hakuna maendeleo ya mradi na hoteli yote imevunjwa na kukosesha mapato serikali kutokana na kutosimamiwa kwa misingi ya utawala wa sheria," alisema Makame. Alisema kuwa bodi ya vileo ilivunjwa kutokana na kushindwa kusimamia sheria namba tisa ya mwaka 2020 baada ya kuruhusu kampuni zaidi ya tatu kuingiza vileo Zanzibar pamoja na kutoa leseni za baa bila ya kuzingatia masharti ya sheria ya umbali wa mita 1000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama shule, nyumba za ibada, madrasa, hospitali na makazi ya watu.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi mpya ya Vileo, Khamis Haji, alithibitisha bodi mpya kuundwa na yeye ndiye mwenyekiti ingawa hakuwa tayari kutaja wajumbe wake.



Mbunge wa Jimbo la Dimani, Mustapha Mwinyi Kondo, akimpa zawadi mwanafunzi Safia Muhamed wa Shule ya Msingi Kisauni ambaye amefaulu mitihani yake ya darasa la sita aliyofanya mwaka jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mbunge ashawishi wazazi kuchangia maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Jimbo la Dimani, Mustapha Mwinyi Kondo, amewataka wazazi na walezi wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kisauni kutokuwa wagumu kuchangia maendeleo ya shule hiyo wakati msaada unapohitajika ili watoto wao wafanya vizuri katika masomo yao.

Aliyasema hayo juzi wakati wa sherehe za kuwaaga walimu wa shule hiyo waliostaafu pamoja na kuwapongeza wanafunzi waliofaulu kipawa maalum (michepuo) waliofanya mitihani yao ya taifa ya darasa la sita mwaka 2020, katika zilizofanyika Shule ya Kisauni Wilaya ya Magharib B Unguja.

Alisema licha ya serikali kutoa elimu bila ya malipo, baadhi ya misaada ya kielimu inahitajika hasa uongozi wa shule unapowataka wazazi na walezi kutoa msaada wao katika kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili shule hiyo.

Alisema baadhi ya wazazi na walezi ni wagumu kuchangia maendeleo ya shule na wapo tayari kugharamika katika shughuli nyingine za kijamii kama harusi wakati elimu ni msingi wa maisha kwa watoto wao.

"Baadhi ya wazazi na walezi wanafanya sherehe za harusi kwa gharama kubwa, lakini kuchangia shule kwa ajili ya maendeleo ya mtoto wake huwa wagumu," alisema.

Pia alisema kuwa walimu wana jukumu kubwa la kuwasimamia wanafunzi ili kufanya vizuri katika masomo yao na kuwa na wataalamu bingwa hapo baadaye.

"Tunafahamu kuwa walimu mnachangamoto nyingi ikiwamo mishahara midogo mnayopata, lakini changamoto hiyo isiwe sehemu ya kutoonyesha bidii zenu katika kutoa elimu kwa watoto wetu," alisema.

Akisoma risala kwa niaba ya walimu wa shule hiyo, Mwalimu Mariyam Masoud, alisema licha ya mafanikio yaliyopatikana shuleni hapo ikiwamo ya ufaulu kwa baadhi ya wanafunzi katika mitihani yao ya taifa, shule inakabiliwa na upungufu wa madarasa hali inayosababisha msongamano, darasa moja lina wastani wa wanafunzi 120.

Alisema hali hiyo inashusha ufanisi katika utendaji kwa walimu na wanafunzi wakati darasa moja linahitajika kuwa na wastani wa wanafunzi 45.

Changamoto nyingine ni uchakavu wa madarasa ambayo baadhi yamejaa vumbi kutokana na kuvunjika kwa saruji iliyowekwa sakafuni na kuhatarisha afya za walimu na wanafunzi.

Kwa upande wake Kaimu Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ahmada Haji, alisema walimu waliostaafu shuleni hapo ni wapishi wazuri wa wanafunzi baadhi yao wamefanikiwa kufaulu mitihani yao ya taifa.

Aliwapongeza wanafunzi wa kike waliofanya vizuri zaidi katika mitihani yao ya taifa mwaka jana ikilinganishwa na wa kiume na kuwataka wanafunzi wote kusoma kwa bidii na kuachana na vitendo viovu ambavyo vitawasababishia kutofikia malengo yao.

Shule ya Kisauni Msingi imeanza rasmi shughuli za ufundishaji mwaka 1992 ikiwa na wanafunzi 325 kati ya hao wanaume ni 167 kwa sasa ina wanafunzi 1,569 wanafunzi wa kike ni 102.

Tangu mwaka 2013 hadi 2020 shule imepasisha wanafunzi 35 wa michepuo na katika sherehe hizo watatu wa kike wamefaulu michepuo mwaka 2020 na kutunukiwa zawadi mbalimbali pamoja na kuwaaga walimu wawili waliomaliza muda wao ya utumishi.

# DC aahidi msako kuungua nyaraka ofisi ya CHADEMA

**Na Thobias Mwanakatwe,** MOMBA

SERIKALI wilayani Momba mkoani Songwe imesema itahakikisha inawasaka na kuwakamata watu waliohusika na kuungua kwa nyaraka katika ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) zilizopo Tunduma mjini.

Mkuu wa Wilaya ya Momba, Fack Lulandala, akizungumza na waandishi wa habari juzi alisema kitendo kilichofanywa na watu hao kinataka kuleta taharuki kwa wananchi ili waone kama Tunduma sio mahali salama wakati sio kweli.

"Tutahakikisha tunawakamata waliohusika bila kujali anatoka chama chake kama amehusika katika tukio hili tutamchukulia hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya alionya watu ambao wameanza kuhusisha tulio hilo la wiki iliyopita na masuala ya kisiasa, na kwamba vyombo vya ulinzi na usalama viachwe vifanye uchunguzi.

Alisema tukio hili linazua maswali mengi kwani lilitokea muda mfupi baada ya walinzi wa ofisi hiyo kuondoka.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Janeth Magomi, aliwaeleza waandishi kuwa (watu wasiojulikana) walivunja ofisi ya CHADEMA Jimbo la Tunduma na kuteketeza kwa moto nyaraka mbalimbali muhimu zilizokuwa ndani ya ofisi hiyo.

Alisema baada ya kupewa taarifa za tukio hilo ambalo lilitokea Oktoba 13 mwaka huu saa 1:00 asubuhi, Jeshi la Polisi na Jeshi la Zimamoto walifika eneo la tukio walibaini ofisi hiyo kuvunjwa na kuchomwa moto kwa nyaraka mbalimbali muhimu za ofisi hiyo.

Kamanda Magomi alitaja vitu vingine vilivyochomwa moto kwenye tukio hilo ni furushi la nguo ambazo zilikuwa pembezoni mwa mlango uliovunjwa.



Ofisa Forodha Mwandamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Muhidini Mwalugoya (aliyesimama), akitoa elimu kuhusu athari za magendo kwa wavuvi wa pwani ya Kilwa Kivinje hivi karibuni, wakati wa kampeni ya utoaji elimu kuhusu athari za magendo katika mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yaamuru aliyekuwa Mwenyekiti NICOL kurudisha gari

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemwamuru aliyekuwa Mwenyekiti wa Kampuni ya NICOL, Felix Mosha, kurejesha mara moja gari la kampuni ya Toyota Land Cruiser na pia kuilipa NICOL Sh. 14,400,000, ikiwa ni gharama zilizotumika kukodisha gari mbadala na kulipa Sh. 22,000,000 kiwango cha pesa ambacho yeye na mdaiwa mwenzake waliuza gari la kampuni bila kibali.

Kesi hiyo ya madai ilisikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga na alitoa hukumu hiyo Oktoba 13, mwaka huu. Katika kesi ya madai iliyosajiliwa kwa namba 282/2017, ilifunguliwa na kampuni ya NICOL dhidi ya Felix Gamaliel Mosha, mwenyekiti aliyeondolewa madarakani na wanahisa na Kathleen Armstrong ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu aliyeondolewa madarakani, ambaye kwa sasa anaishi Marekani.

Katika kesi hiyo, Hakimu alisema mahakama yake ilithibitisha kwamba kwa mujibu wa vilelezo pamoja na ushahidi uliotolewa, walalamikiwa waliondolewa kihalali na wanahisa kwenye nafasi zao wakati wa mkutano mkuu wa wanahisa kwa ubadhirifu wa mali za kampuni.

Mahakama ilitoa uamuzi huo baada ya kuthibitisha kuwa sababu zilizotolewa na walalamikiwa kwamba walirudishwa madarakani katika uamuzi uliotolewa na Jaji, Dk. Fauz Twaibu (kwa sasa mstaafu) katika ya madai namba 16/ 2011 si ya kweli na yenye kupotosha, kwa kuwa uamuzi wa Jaji Twaibu ulisema wazi kwamba, amri yake isingeweza kuwa ya kudumu na hasa baada ya wanahisa kufikia uamuzi wa kuwaondoa madarakani walalamikiwa na kuteua viongozi wapya, amri ile ilikufa.

Hakimu alisema mahakama imeamua uamuzi wa wanahisa wa kuchagua viongozi wengine ulikuwa ni halali na ndiyo maana uamuzi huo ulikubaliwa kama ilivyothibitishwa na maamuzi mbalimbali ya mahakama Kuu, pia maamuzi hayo ya wanahisa ya Aprili 14, 2012, hayajawahi kubadilishwa na mahakama yoyote mpaka sasa.

Alisema mahakama imeamua Mosha na Armstrong warejeshe mara moja gari ya kampuni Namba T. 133 AVG, Toyota Land Cruiser na pia kuilipa NICOL, jumla ya Sh. 14,400,000 kama gharama zilizotumika kukodisha gari mbadala, kulipa Sh. 22,000,000 kiwango cha pesa alichouza gari ya kampuni bila kibali na pesa hizo kutokuonekana kwenye vitabu vya fedha vya kampuni, gharama za usumbufu Sh. 10,000,000 pamoja na gharama za kesi.

Katika kesi hiyo Kampuni ya NICOL iliwakilishwa na Wakili Benjamin Mwakagamba wa Ofisi ya BM Attorneys wakati Mosha aliwakilishwa na Wakili Dominic Daniel.

# PPRA yatoa mafunzo usimamizi mikataba

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKATI zaidi ya asilimia 70 ya bajeti ya fedha za serikali ikitumika kwa ajili ya ununuzi wa umma, bado kuna changamoto ya usimamizi wa mikataba na fedha nyingi imeendelea kupotea kutokana na kutokusimamiwa vyema.

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeamua kuwajengea uwezo wasimamizi wa mikataba hiyo ikiwa ni jitihada za kupata uelewa ili kuokoa fedha za serikali zisipotee.

Akizungumza katika mafunzo hayo ya kupata uelewa wa usimamizi wa mikataba na elimu ya ununuzi yaliyohusisha Taasisi na Mashirika ya Umma, Ofisa Manunuzi Mkuu wa PPRA, Gilbert Kamde, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba Saba ya Mwaka 2011 pamoja na maboresho yake yaliyofanyika mwaka 2016 na usimamizi wa mikataba, wadau wote wanapaswa kuwa na uelewa huo ili kuhakikisha fedha hizo za serikali zinatumika kwa taratibu zilizopo.

Alisema tangu maboresho yake yafanyike baadhi ya wadau hawajapata elimu yake na kuamua kuwapatia mafunzo hayo ili kuwawezesha kuwa na uelewa mzuri katika sekta ya manunuzi ya umma pamoja na kutekeleza mikataba.

Naye Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu PPRA, Mhandisi Mary Swai, alisema wameamua kutoa elimu hiyo ya sheria hizo kwa makundi maalumu kwa kuwa wengine wao hivi sasa wamekuwa wakijihusisha na shughuli za ujasiriamali lakini hawazifahamu.

Alitaja moja ya kundi hilo maalumu ni jamii ya viziwi katika Mkoa wa Morogoro, lengo ni kuhakikisha linapata fursa ya kuomba zabuni kwa kufuata sheria zilizopo.

"Sisi kama PPRA tumeona haya makundi maalumu hivi sasa yanajishughulisha na ujasiriamali, lakini hawajui sheria za manunuzi hivyo tumeamua kutoa mafunzo waweze kufuata sheria hizo ambazo katika sekta ya manunuzi ni muhimu sana sasa tumeanza na viziwi na tutaendelea na makundi mengine," alisema Mhandisi Swai.

Alisema serikali inayatumbua makundi maalum ikiwamo viziwi na kwamba sheria ya ununuzi wa zabuni unazitaka taasisi kuhakikisha asilimia 30 ya waombaji wa zabuni inayotangazwa wanakuwa watu wenye kundi husika.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAMAVITA), Kelvin Nyema, alisema elimu hiyo itawawezesha kukuza uelewa wa sheria za ununuzi bidhaa mbalimbali hatua itakayowezesha kundi hilo kushiriki katika ununuzi wa zabuni.

Alisema pamoja na kundi hilo kufanya shughuli hiyo ya ujasiriamali, wengi wao wanafanya bila kufuata sheria za manunuzi na kupitia mafunzo hayo watapata uwelewa na kufuata sheria ya ununuzi.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Morogoro, Jesca Kagunila, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya ukombozi wa kundi hilo la viziwi kuweza kuongeza ulewa wa kufuata sheria za kuomba zabuni mbalimbali.

Mafunzo hayo yametolewa mkoani hapa yakihusisha washiriki 60 kutoka halmashauri zote za mkoa huo.

**MAKALA**

# Jinsi Lipa-Kulingana-na-Matokeo inavyowezesha upatikanaji fedha kwa sekta ya maziwa Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**



Maofisa mifugo wakiwamwagia dawa ng'ombe kwa ajili ya kuwakinga na maradhi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UPATIKANAJI wa fedha ni muhimu katika kusaidia na kupanua biashara; vinginevyo wanapungukia mzunguko wa fedha unaohitajika katika uwekezaji na usambazaji wa bidhaa na huduma kwa wateja wao. Wakati mwingine, upatikanaji mdogo wa fedha unatosha kukandamiza soko lote.

AgResults, mpango wa dola milioni 152 unaobuni na kutekeleza mashindano ya tuzo za Lipa-Kulingana-na-Matokeo ili kuhamasisha sekta binafsi kuepuka kushindwa kwa soko la kilimo, ukijifunza umuhimu wa upatikanaji wa fedha kupitia mashindano yake ya Nigeria (2013-2019) ambayo yalihimiza wakulima wadogo wa mahindi kutumia teknolojia ya kudhibiti sumukuvu (Aflasafe).

Mapema, wakulima wengi wa mahindi walishindwa kumudu ununuzi wa Aflasafe. Ni wale tu walioweza kutambua na kupata fedha walimudu upatikanaji wa Aflasafe na pembejeo zingine zinazohitajika katika uzalishaji wa mahindi yenye ubora. Kwa maneno mengine, upatikanaji wa fedha ulifungua milango ya mafanikio.

BIASHARA YA MAZIWA NA BENKI

Shukrani kwa somo kutoka Nigeria na miradi yake mingine, AgResults imechukua hatua madhubuti ya kuongeza upatikanaji wa fedha katika mradi wake wa Kuchagiza Uzalishaji wa Maziwa Tanzania (2019-2023), ambao unatoa zawadi kwa wasambazaji wa pembejeo kutoka sekta binafsi na wasindikaji wa maziwa, kutoa vifurushi vya pembejeo za udhibiti wa vimelea, lishe, chanjo pamoja na huduma za ugani - kwa wakulima wadogo ili kuongeza ubora na wingi wa uzalishaji wa maziwa.

Kwa kuzingatia biashara nyingi za ndani nchini Tanzania kihistoria zilikabiliwa na kikwazo katika upatikanaji wa mikopo, mpango wa AgResults ulitambua ilikuwa ni muhimu kuwashirikisha wadau katika mnyororo wa thamani ili kujenga mazingira mazuri ya kuwezesha upatikanaji wa fedha.

Pamoja na wawakilishi wa serikali, wawakilishi wa wafadhili na washindani wenye uwezo, taasisi za kifedha zilialikwa kwenye uzinduzi wa mradi mnamo Novemba 2019, ambapo walijifunza juu ya lengo la mradi na muundo wa tuzo.

Kupokea rasmi taarifa hii kulihakikishia benki kwamba tuzo hiyo ilikuwa halali na ilionyesha kuwa inaweza kuwa na thamani ya kutoa mikopo kwa biashara zilizokidhi vigezo.

Katika hafla hiyo, Benki za NMB na CRDB ziliwasilisha kuhusu mikopo ya vifaa vinavyopatikana washiriki wa shindano kulingana na shughuli zao za biashara na pia walizungumza nao mmoja baada ya mwingine kuhusu mchakato wa mkopo.

Wakiwa wamewezeshwa na maarifa haya, wauzaji wa pembejeo walitathmini uwezo wao wa kufadhili shughuli wakati wa ushindani na kufanya hesabu ya msingi wao wa wateja waliopo na wateja wapya wenye uwezo wa kupima uwekezaji unaohitajika ili kuwezesha maombi yao ya mkopo.

Matokeo ya tathmini yaliwalazimu washindani kufikiri zaidi juu ya jinsi ya kupata fedha za kuunga mkono ahadi zilizofanywa walipochagua kushiriki katika ushindani. Matokeo pia yalionyesha kampuni jinsi ya kutoa ufumbuzi zaidi wa matatizo ya wateja wao.

**DAMIAN 'ALIVYOTOKA' KIUCHUMI**

Akipatikana mkoani Morogoro, Damian Agrovet ameuza pembejeo za kilimo na kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa maziwa kwa miaka 18. Kabla ya ushindani wa AgResults, Damian hakuweza kupata rasilimali sahihi za kifedha kufanya uwekezaji katika malisho, chakula cha bora cha mifugo na mnyororo sahihi kwa huduma za kisasa za upandikizaji (AI).

Hata hivyo, kutokana na mbinu madhubuti ya ushindani wa kuunganisha biashara na benki, Damian alikuwa na sifa zote stahiki na hivyo NMB ikampa mkopo wa Sh. milioni 17 kusaidia kutimiza malengo ya biashara.

Kupitia mkopo huo, Damian alinunua tangi la Kg 35 kwa ajili ya kuhifadhi kioevu cha nitrojeni, matangi mawili yenye Kg tatu kwa ajili ya utoaji wa huduma za upandikizaji, na pikipiki ili kuhakikisha kuwa huduma za upandikizaji zinatolewa kwa wakati. Miundombinu hii ilimwezesha Damian kusajili miamala 81 ya upandikizaji katika kipindi cha miezi minne, na kusababisha mimba kwa ng'ombe 37 waliopotiwa.

Damian Agrovet pia alitumia sehemu ya fedha kununua nyasi na malisho ili wakulima wake waweze kupata lishe kamili kwa vigezo vinavyotakiwa katika mashindano hayo. Ili kuwasaidia wakulima wengi zaidi wa mbali kupata nyasi kwa bei ya ushindani, Damian alibadilisha mkopo wa kuendeleza chakula cha maziwa cha gharama nafuu na mahitaji ya kawaida kwa msaada kutoka TanFeeds International, kampuni ya utengenezaji wa malisho.

Pamoja na hayo, Damian alihimiza matumizi ya chakula bora cha mifugo ili kuboresha uzalishaji wa maziwa na lishe kwa ng'ombe, akiwaandaa kwa huduma za upandikizaji.

Wakati wa kipindi cha kwanza cha mauzo (Julai 17, 2020 - Aprili 16, 2021), Damian alitoa Kg 77,133.5 za chakula bora cha mifugo kupitia miamala 552 ya mauzo. Damian aliuza Kg 6,600 za chakula bora cha mifugo Desemba 2020 na Kg 24,500 Januari mwaka huu, kisha kuuza vifaa 98 vya kuhifadhia mbegu kwa ajili ya upandikizaji wa mimba kati ya Januari na Februari. Hii iliendelea hadi mwisho wa kipindi cha mauzo.

**MAFANIKIO SEKTA YA MAZIWA**

Mafanikio ya muda mrefu ya upatikanaji wa fedha yanakwenda zaidi ya mauzo ya pembejeo. Kwa kuitafutia ufumbuzi mapema changamoto ya upatikanaji wa fedha kwenye mashindano, AgResults imemwezesha Damian Agrovet na wasambazaji wengine kujenga uhusiano endelevu na benki na kuzitumia zawadi kulipia mikopo na kuboresha shughuli zao.

Ni mtaji huu pia unawasaidia wafanyabiashara kutanua upatikanaji wa pembejeo kwa ajili ya wakulima wadogo, kuongeza uzalishaji na kuimarisha sekta ya maziwa kwa ujumla nchini Tanzania.

# VARANE WA SIMBA ABEBA TUZO BEKI BORA LIGI KUU DR CONGO

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akiendelea kupigania namba kuingia kikosi cha kwanza, beki mpya wa Kati wa Simba, Henoc Inonga Baka 'Varane', aliyejiunga na Klabu ya Simba akitokea DC Motema Pembe ya kwao DR Congo, amechaguliwa kuwa Beki Bora wa Ligi Kuu ya nchini humo.

Varane bado hajaweza kupora nafasi moja kutoka kwa mabeki wa kati wa Simba, Muivory Coast Pascal Wawa ama Mkenya Joash Onyango wanaounda safu ya ulinzi ya timu hiyo wakisaidiwa na mabeki wa pembeni Shomary Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Lakini katika tuzo za msimu uliomalizika wa 2020/21 Ligi Kuu DR Congo juzi, Varane alitangazwa kuwa beki bora wa msimu huo huku aliyekuwa Kocha Mkuu wa AS Vita (kwa sasa RS Berkane ya Morocco), Florent Ibenge, akitangazwa kuwa Kocha Bora wa msimu.

Hata hivyo, Varane ambaye anauwezo mkubwa wa kucheza mipira ya juu na chini kwa umakini mkubwa, huku akimudu kutoa pasi mpenyezo kwa kiwango cha juu, bado ana uwanja mpana wa kumshawishi Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didie Gomes kumchomoa beki mmoja kati ya Wawa ama Onyango.

Kwa baadhi ya mechi ambazo Varane amecheza kwa dakika chache, ameonyesha kuwa na uwezo mkubwa si tu kucheza mipira ya juu na pasi mpenyezo za uhakika, bali pia ni beki mwenye kasi na anayejua vema kuanzisha mashambulizi.

Beki huyo ambaye jana alianza kikosi cha kwanza sambamba na Wawa kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini nchini Botswana dhidi ya Jwaneng Galaxy FC anapewa nafasi kubwa ya kuibeba Simba katika michuano hiyo.

Timu hizo zinatarajia kurudiana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili ijayo na itakayopata matokeo ya jumla itatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Simba inapewa nafasi kubwa ya kusonga mbele kutokana na kufanya vizuri msimu uliopita kwa kufika robo fanali kabla ya kutolewa na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

## TUPO TAYARI...




Wachezaji wa Yanga wakielekea kukwea pipa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), tayari kwa safari ya Songea kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya KMC FC itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Majimaji. **PICHA: YANGA**

# Ndayiragije akerwa sare na Mtibwa

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumalizika kwa mechi kati ya Geita Gold dhidi ya Mtibwa Sugar juzi, na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1, Kocha Mkuu wa 'Wachimba Madini' hao, Etienne Ndayirajige, alionekana akiwa na hasira na kwenda moja kwa moja kumuwakia straika wake, Daniel Lyanga kwa dakika kama moja hivi.

Lyanga ambaye ndiye mfungaji kwenye mechi hiyo, alilazimika kumsikiliza kocha wake kwa makini aliyeonekana ni kama hajaridhishwa na yaliyokuwa yakiendelea uwanjani.

Alipouliza ni kitu gani alikwenda kumwambia straika wake huyo kutokana na kuoneka akimfokea, Ndayiragije alisema kuwa hiyo ni siri ya chumba cha kubadilishia nguo na hawezi kuyasema aliyokuwa akimwambia mchezaji wake.

"Hapa siwezi kusema kama kocha, haya yanabaki kuwa ni siri yetu. Ni mambo ya kwenye chumba cha kubadilishia nguo na tutayamaliza huko huko," alisema kocha huyo.

Akizungumzia mechi hiyo ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Nyankumbu, Geita, kocha huyo alisema ingawa ushindi ulikuwa mikononi mwao, lakini ameridhika na sare ambayo wameipata, hivyo wanaangalia mechi ijayo.

"Siku zote mimi ni mshindani, huwa nahitaji ushindi, ndiyo maana umeona ni kama sijaridhika hivi na sare, lakini kama tayari tumeshaipata hakuna cha kufanya, hata ukiangalia Mtibwa Sugar nao leo walicheza vizuri sana," alisema.

Geita Gold ingeweza kuondoka na ushindi kwenye mechi hiyo kama penalti ya dakika za mwisho kupitia kwa Raymond Masota ingezama nyavuni, lakini kipa Aboutwalib Msheli alipangua na kufanya mchezo huo kumalizika kwa sare.

## Kidali sasa M/kiti Bodi ya Ligi Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VIONGOZI wa klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar wamemchagua Haji Issa Kidali kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Zanzibar (ZPL).

Katika uchaguzi huo uliofanyika juzi na kusimamiwa na Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Kidali alikuwa mgombea pekee kwenye nafasi hiyo na wajumbe wote 12 walimpigia kura zote za ndio hivyo kushinda kwa asilimia 100.

Kwa upande wa mjumbe wa bodi hiyo kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda, wajumbe walimchagua Ali Juma Khamis kutoka Kanda ya Pemba kwa kupata kura nane kati ya wajumbe 12 waliopiga kura katika uchaguzi huo, ambao wajumbe wanne hawakuhudhuria.

Akizungumza baada ya kuwatangaza viongozi walioshinda katika uchaguzi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ZFF, Fadhil Ramadhan Mberwa, aliwataka viongozi waliochaguliwa kusimamia majukumu yao pamoja na kufanya kazi kwa ushirikiano.

Uchaguzi huo umefanyika baada ya aliyekuwa Mwenyekiti wa bodi hiyo, Mohmed Kassim, kuondolewa na klabu kwa kumpigia kura ya kutokuwa na imani naye mapema mwanzoni mwa mwaka huu.

## Usajili wa mtandao Ligi Kuu Z'bar wakamilika

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), bado inaendelea na mchakato wa kupitisha fomu za usajili na uhamisho wa wachezaji kuelekea msimu mpya wa ligi hiyo unaotarajiwa kuanza baadaye mwezi huu.

Zoezi hilo linafanyika ikiwa ni baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili Oktoba 11, mwaka huu na ZFF kutoongeza muda wa ziada wa kufanya usajili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa ZFF, Mohamed Kabwanga, alisema klabu zote za Zanzibar kuanzia ngazi ya mikoa na wilaya zimefanya usajili huo kwa njia ya mtandao.

Alisema katika zoezi hilo, changamoto zilizojitokeza ni za kawaida kwa klabu za ngazi za wilaya na mikoa ikiwamo kutokuwa na wataalamu wa TEHAMA katika klabu zao.

Aidha, alisema zoezi hilo la uhamisho wa wachezaji kwa njia ya mfumo limefanikiwa kwa asilimia kubwa kama ambavyo (ZFF) ilikusudiwa.

"Klabu zote za Zanzibar kwa sasa zipo katika mfumo wa ZFF na ndizo zitakazoruhusiwa kucheza ligi, mabadiliko haya ya mfumo yalianza tangu msimu uliopita, lakini ilikuwa kwa madaraja machache ila msimu huu ni kwa madaraja yote," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAZARD CHAMBO YA SALAH

REAL Madrid watamuuza kiungo wao wa kati, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 30, ili kupata fedha kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29. **(Ekrem Konur)**

### HAALAND NDANI YA NEWCASTLE

NEWCASTLE United wanamsaka mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland, huku Real Madrid, Manchester City na Paris St-Germain wakimtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 21. **(AS, via Sport Witness)**

### UNITED WATENGA PAUNI MIL 70

MANCHESTER United imetenga pauni milini 70 kwa ajili ya dirisha lijalo la uhamisho, ambazo zitatumika kuimarisha kikosi hicho kwenye mbio za Ligi Kuu England. **(Star Sunday)**

### JOVIC KUMRITHI LACAZETTE

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Luka Jovic mwenye umri wa miaka 23, anatazamwa kuchukua nafasi ya mshambuliaji, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30 kule Arsenal. **(Fichajes)**

### WILSHERE AMSHAURI RICE

KIUNGO wa kati wa zamani wa Arsenal, Jack Wilshere mwenye umri wa miaka 29, amemshauri mlinzi wa England, Declan Rice, 22, akatae ofa za uhamisho kutoka Manchester United na Chelsea na aendelee kubakia West Ham. **(Mirror)**

### ODEGAARD YUPO TAYARI

KIUNGO wa kati wa Arsenal na nahodha wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, yuko tayari kupokea wazo la kurejea katika klabu ya Real Sociedad, amesema golikipa wa zamani wa 'Washikabunduki', Mat Ryan mwenye umri wa miaka 29, ambaye kwa sasa anacheza katika klabu hiyo ya nchini Hispania. **(Mundo Deportivo, via Mirror Online)**

### LEWANDOWSKI NJIA NYEUPE CITY

WAKALA wa Robert Lewandowski, 33, amesema mshambuliaji huyo wa Poland na Bayern Munich kuwa Manchester City ndio "timu anayoweza kuhamia" kwa siku zijazo. **(Bild, via Star Online)**

### KOUNDE AITAKA MAN UNITED

MLINZI wa Klabu ya Sevilla, Jules Kounde, amemuomba wakala wake kufanya mazungumzo na Manchester United, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22 pia akilengwa na klabu za Chelsea na Real Madrid. **(El Nacional)**

### USAJILI PAUNI MILIONI 40

NEWCASTLE wamepanga bajeti ya pauni milioni 50 tu kwa ajili ya dirisha la kwanza la uhamisho chini ya wamiliki wao wapya Wasaudia. **(Sunday Telegraph)**

### WAKALA AMFUATA SALAH

WAKALA wa Mohamed Salah amesafiri hadi Liverpool kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya ana kwa ana kuhusu mkataba mpya wa nyota huyo. **(Mirror, via Star Online)**

### ALVES ATAKA KURUDI BARCA

MLINZI wa zamani wa Barcelona, Dani Alves amejitolea kujiunga tena na klabu hiyo kwa mkataba wa 'gharama ya chini'. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 38, sasa yuko huru baada ya kusitisha mkataba wake na Sao Paolo katikati ya Septemba. **(AS)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER AKIRI KUFANYA MAAMUZI MABAYA UTD

## Ni wakati wakichezea kichapo kutoka kwa Leicester City, asema hatukustahili kushinda, maana tulicheza kwa...

**LONDON, England**

OLE Gunnar Solskjaer amekubali kwamba, "nilifanya maamuzi mengi mabaya" wakati Manchester United ikichezea kichapo cha mabao 4-2 kutoka kwa Leicester City pale kwenye Uwanja wa King Power, kwenye mechi ya Ligi Kuu England, Jumamosi.

Kupoteza mchezo huo kumeifanya Man United kuhitimisha umwamba wake wa kucheza mechi 29 bila kupoteza katika Ligi Kuu na pia kuambulia pointi moja tu katika mechi zake tatu zilizopita.

Vijana hao wa Solskjaer walianza kuongoza, lakini baadaye wakaruhusu kufungwa bao la tatu na baadaye kuruhusu la nne katika dakika ya mwisho ya mchezo huo.

Kocha huyo raia wa Norway hakuwa na furaha kutokana na mabao matatu waliyofungwa kwa haraka, lakini alikubali kubeba lawama zote kwa kupoteza mchezo huo.

Matokeo hayo sasa yameifanya Man United kuwa imeshinda mchezo mmoja tu kati ya mitano iliyopita kwenye mashindano yote, ikipoteza mara tatu.

"Ukiangalia mchezo wenyewe, mabao yote manne tuliyofungwa yalikuwa ya kizembe," alisema Solskjaer akiiambia Sky Sports.

"Hatukustahili kushinda, maana tulicheza kwa kiwango cha chini mno. Kiwango chetu hakikuwa kizuri kabisa. "Tulipata bao zuri sana lililofungwa na Mason (Greenwood) na alikuwa anagonga mlango kwa ajili ya bao jingine, lakini tukaruhusu kufungwa kirahisi.

"Wenetu walitengeneza nafasi nyingi za kufunga. Mabao mawili ndani ya dakika mbili yalitumaliza kabisa na lile la (Jamie Vardy) lilitupotezea kabisa umakini wetu.

"Nilichagua timu na Harry (Maguire) hakuonyesha chochote kutokana na majeraha yanayomsumbua.

"Pengine nilifanya makosa makubwa sana na nakubali kwamba makosa yalikuwa ya kwangu mwenyewe."


Licha ya matokeo hayo mabaya kwa United, Solskjaer amesisitiza bado ana imani kubwa kwa kikosi chake.

"Kila wakati unapopoteza inakuwa ni nafasi ya kujipanga upya, na sisi tunaishi kwa namna hiyo," alisema Solskjaer akiiambia BBC.

United ina nafasi ya kurekebisha makosa yake, Jumatano itakapocheza na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Atalanta kwenye mchezo wa makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

MECHI KALI
HOME
AWAY
ARSENAL
1.71 | 3.73 | 4.97
CRYSTAL PALACE
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO



# GUARDIOLA AANIKA BURNLEY ILIPOWATESA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola aliachwa na furaha kubwa namna timu yake, Manchester City ilivyocheza kwa kiwango bora na kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Burnley pale kwenye Uwanja wa Etihad, Jumamosi.

City imeshinda mechi tano zilizopita dhidi ya Burnley kwa mabao 5-0, lakini juzi walionekama kuwa kwenye wakati mgumu baada ya Bernardo Silva kufunga bao la ufunguzi.

Hilo lilikuwa bao la saba la Silva dhidi ya Burnley katika mechi nane za Ligi Kuu - akiwa ameifunga mabao mengi zaidi timu hiyo kuliko mchezaji yeyote.

Hata hivyo, Kevin De Bruyne alifunga zikiwa zimesalia dakika 20 mchezo kumalizika na kuwahakikishia City ushindi huo.

Ingawa sasa Man City wana mechi sita ambazo hawajaruhusu bao kati ya nane za Ligi Kuu msimu huu, Guardiola anatambua kwamba, timu yake inahitaji kupambana zaidi.

"Tunakimbia na kupambania kila mpira," alisema akiambia BBC Sport.

"Burnley walicheza mipira mirefu na walicheza kwa kasi zaidi na hivyo ilitulazimu kujilinda zaidi."

# Mane afikisha mabao 100 bila penalti



**LIVERPOOL, England**

SADIO Mane amefikisha mabao 100 aliyofunga kwenye Ligi Kuu England, huku nyota huyo wa Liverpool akifanya hivyo bila bao lolote la penalti.

Mane alifunga bao kwa kuunganisha pasi ya Mohamed Salah kwenye mchezo wa Jumamosi dhidi ya Watford wakati wakiibuka na ushindi wa 5-0 na kufikisha idadi hiyo ya mabao.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Senegal alifunga bao lake la kwanza kwenye ligi hiyo Oktoba mwaka 2014 alipotupia la ushindi wakati Southampton wakiwafunga Stoke City 1-0.

Alifunga mabao mengine tisa msimu huo na kufuatiwa na 11 kwenye msimu wa 2015-16, na akajikuta akiivutia Liverpool iliyomsajili kwa pauni milioni 34.

Wakati wengine walikuwa wanamtilia shaka mwanzoni, Mane alizoea haraka mazingira na alifunga mabao 13 kutoka mechi 27 za Ligi Kuu kwenye msimu wake wa kwanza.

Alifunga mabao zaidi ya 10 katika kila msimu kwa msimu yake mitano iliyopita na 'Wekundu' hao kwenye Ligi Kuu, huku msimu wa 2018-19 ukiwa bora zaidi kwake.


Mafanikio ya Mane kwa kufikisha idadi hiyo ya mabao yamenogeshwa na ukweli kwamba, hakuna hata moja la penalti kati ya hayo 100.

Yeye ni mchezaji wa 31 kufikisha mabao 100 kwenye Ligi Kuu, lakini ni wa tatu kufunga idadi hiyo bila bao la penalti, akiungana na Les Ferdinand (149) na Emile Heskey (110).

Mane pia ni mchezaji wa tatu kutoka Afrika kufikisha idadi hiyo ya mabao baada ya Didier Drogba na mchezaji mwenzake, Salah.

LIVE IN PLAY

# GIROUD AJIWEKEA REKODI YAKE MILAN



**MILAN, Italia**

OLIVIER Giroud alifurahia kurudi uwanjani na kufunga bao wakati Milan ikipambana kutoka nyuma na kuifunga Hellas Verona mabao 3-2 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia katika Uwanja wa San Siro, Jumamosi iliyopita.

Rossoneri walionekana watapoteza mchezo wao huo wa kwanza nyumbani katika mechi 30 za Serie A, wakati Verona walipokuwa mbele kwa mabao mawili ya Gianluca Caprari na Antonin Barak kabla ya mapumziko.

Giroud akafunga kwa kichwa na kurudisha matumaini kwa Milan, huku Franck Kessie akisawazisha kwa mkwaju wa penalti, kabla ya Koray Gunter kujifunga.

Matokeo hayo yamekifanya kikosi cha Stefano Pioli kupaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo mbele ya Napoli ambao walikuwa wanacheza jana, Jumapili na Torino.

Kwa kufunga bao lake la tatu kwenye mechi mbili za kwanza za Serie A nyumbani, Giroud alifikia rekodi ambayo awali iliwekwa na Oliver Bierhoff, Alexandre Pato, Mario Balotelli na Carlos Bacca.

Nyota huyo wa zamani wa Arsenal na Chelsea, ambaye alikosa mechi nne kati ya tano zilizopita za Milan, alikubali kwamba umekuwa ni muda mrefu kurudi kwenye orodha ya wafungaji.

"Nilisubiri kwa muda mrefu kuwa katika wakati huu. Nilimisi mashindano," alisema Giroud, ambaye mara ya mwisho alifunga katika ushindi dhidi ya Cagliari, Agosti, akiiambia DAZN.

"Katika kipindi cha kwanza, tulitakiwa kufanya vizuri, lakini tulijikuta tupo nyuma. Bado sijihisi kuwa fiti kwa asilimia 100, lakini naona naimarika kila siku."

# Kiwango cha Mendy chamkuna Tuchel



**LONDON, England**

EDOUARD Mendy alitakiwa kujumuishwa kwenye orodha ya wanaowania Ballon d'Or, lakini Thomas Tuchel ana matumaini jambo hilo halimkwazi golikipa huyo wa Chelsea.

Kipa huyo wa kimataifa wa Senegal, Mendy alicheza mechi tisa bila kuruhusu bao wakati Chelsea ikitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita - ikiwa ni idadi nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote kwenye mashindano hayo.

Aliokoa hatari kwa asilimia 91.2 pia aliongoza kati ya magolikipa waliocheza angalau mechi sita kwenye msimu wa 2020-21 katika mashindano hayo.

Wakati wachezaji wenzake wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, Jorginho, N'Golo Kante na Mason Mount walitajwa kwenye orodha ya wachezaji 30 wanaowania tuzo ya Ballon d'Or, Mendy ameachwa.

Na katika mchezo wa Jumamosi wa Ligi Kuu wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Brentford, aliokoa hatari sita na kufikisha mechi 20 alizocheza bila kuruhusu bao kati ya 38.

Tuchel anaamini Mendy anatakiwa kutambulika kwa kiwango chake na hivyo anahitaji kutunukiwa tuzo yake binafsi, lakini hadhani kama kipa wake huyo atakuwa analifikiria sana hilo.

Alipoulizwa kama Mendy alitakiwa kuwa kwenye orodha hiyo, Tuchel aliwaambia waandishi wa habari: "Ndio, lakini nina furaha na muhimu zaidi ni kiwango chake kuliko hiyo orodha.

"Sidhani kama hilo linamsumbua, natumaini halimkwazi kabisa, kwa sababu hata mimi silifikirii, ninachoangalia ni kiwango chake na anavyoisaidia timu."


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA





## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 18 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 1488 | Unirea Dej vs Hermanstadt | 4.55 | 3.00 | 1.85 |
| 16:00 | 5704 | Radnicki Nis vs FK Radnicki 1923 | 1.54 | 4.06 | 5.03 |
| 17:30 | 4181 | Botosani vs Chindia Targoviste | 2.09 | 2.99 | 3.73 |
| 18:00 | 1613 | Doxa Katokopia vs Aris Limassol | 3.07 | 3.02 | 2.42 |
| 18:00 | 1791 | NK Celje vs ASK Bravo | 2.17 | 3.45 | 2.91 |
| 18:00 | 3534 | Metalac vs Mladost Lucani | 2.61 | 3.04 | 2.61 |
| 19:00 | 3403 | Stal Mielec vs Zaglebie Lubin | 2.66 | 3.10 | 2.52 |
| 19:00 | 4582 | Apoel Nicosia vs Ethnikos Achnas | 1.27 | 5.55 | 9.90 |
| 19:00 | 4664 | Real Garcilaso vs Deportivo Municipal | 2.76 | 3.15 | 2.41 |
| 19:30 | 1000 | Lamia vs Aris Salonica | 3.84 | 3.10 | 2.03 |
| 19:30 | 2339 | Chernomorets Odessa vs Veres Rivne | 2.53 | 3.21 | 2.58 |
| 20:00 | 1680 | Orgryte IS vs Trelleborgs FF | 2.47 | 3.29 | 2.84 |
| 20:00 | 1920 | Aarhus vs Aalborg | 2.51 | 3.20 | 2.75 |
| 20:00 | 1937 | Osters IF vs Vasalunds IF | 1.60 | 3.99 | 5.38 |
| 20:00 | 2090 | Hatayspor vs Gaziantep BB | 1.76 | 3.69 | 4.23 |
| 20:00 | 2100 | GIF Sundsvall vs Akropolis IF | 1.60 | 3.94 | 5.58 |
| 20:00 | 2250 | Alanyaspor vs Kayserispor | 1.65 | 3.95 | 4.64 |
| 20:00 | 3643 | CSKA 1948 vs Beroe | 2.29 | 3.24 | 2.85 |
| 20:00 | 3833 | BK Hacken vs Norrkoping | 2.47 | 3.34 | 2.56 |
| 20:00 | 4489 | Istanbulspor vs Tuzlaspor | 2.22 | 3.20 | 3.01 |
| 20:00 | 4615 | Djurgardens IF vs Elfsborg | 1.84 | 3.63 | 3.63 |
| 20:00 | 5545 | Alaves vs Betis | 3.51 | 3.31 | 2.14 |
| 20:30 | 1749 | FC Trollhattan vs Skovde Aik | 1.82 | 3.62 | 3.72 |
| 20:30 | 3979 | Universitatea Craiova vs Clinceni | 1.46 | 3.91 | 7.24 |
| 20:45 | 5980 | Hapoel Tel Aviv vs Beitar Jerusalem | 2.25 | 3.05 | 3.10 |
| 21:00 | 2082 | Jong Utrecht vs Roda Kerkrade | 3.51 | 3.71 | 1.88 |
| 21:00 | 2388 | El Porvenir vs General Lamadrid | 2.71 | 2.76 | 2.76 |
| 21:00 | 3270 | Juventud Unida SM vs Argentino Rosario | 2.76 | 2.81 | 2.66 |
| 21:00 | 3543 | San Telmo vs Deportivo Moron | 2.26 | 2.85 | 3.33 |
| 21:00 | 4351 | FC Volendam vs NAC Breda | 1.61 | 4.19 | 4.48 |
| 21:00 | 4482 | Central Ballester vs Defensores Cambaceres | 3.88 | 2.91 | 2.03 |
| 21:00 | 4532 | Jong PSV vs Telstar | 2.04 | 3.57 | 3.18 |
| 21:00 | 4674 | Deportivo Muniz vs Centro Espanol | 2.81 | 2.81 | 2.61 |
| 21:00 | 5846 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Ajax | 2.97 | 3.80 | 2.06 |
| 21:15 | 2195 | Escuela Municipal Deportivo Binacional vs Universitario | 3.20 | 3.39 | 2.05 |
| 21:15 | 5966 | Shamrock Rovers vs Bohemians FC | 1.67 | 3.58 | 4.65 |
| 21:30 | 1662 | Deportivo Riestra vs Gimnasia Mendoza | 2.61 | 2.81 | 2.81 |
| 21:30 | 3152 | Jagiellonia vs Radomiak Radom | 2.35 | 3.09 | 2.90 |
| 21:35 | 4116 | CA Atlanta vs CA Tigre | 3.10 | 3.01 | 2.27 |
| 21:45 | 2748 | Venezia vs Fiorentina | 4.01 | 3.61 | 1.89 |
| 21:45 | 3400 | Nimes vs AC Ajaccio | 2.39 | 2.86 | 3.26 |
| 22:00 | 1024 | Guabira Montero vs Nacional Potosi | 1.52 | 4.17 | 5.04 |
| 22:00 | 1950 | Tombense MG vs Novorizontino SP | 2.65 | 2.89 | 2.70 |
| 22:00 | 2054 | Tigres FC (COL) vs Llaneros FC | 3.12 | 2.79 | 2.40 |
| 22:00 | 2442 | Renate vs Pro Vercelli | 2.45 | 3.12 | 2.93 |
| 22:00 | 3197 | Espanyol vs Cadiz CF | 1.63 | 3.70 | 5.81 |
| 22:00 | 4035 | Orsomarso vs Union Magdalena SM | 3.21 | 3.16 | 2.14 |
| 22:00 | 5320 | Arsenal vs Crystal Palace | 1.71 | 3.73 | 4.97 |
| 23:00 | 3469 | Excursionistas vs Sportivo Dock Sud | 2.25 | 3.10 | 3.05 |
| 23:30 | 5122 | Cesar Vallejo vs Sport Huancayo | 1.94 | 3.29 | 3.62 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Oktoba 18, 2021
Nipashe



Solskjaer akiri kufanya maamuzi mabaya UTD

UKURASA 21

CHA PILI...



John Bocco akipongezwa na wachezaji wenzake, Sadio Kanoute (aliyemkumbatia), Henoc Inonga 'Varane' (kushoto) na Taddeo Lwanga, baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati Simba ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy FC kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Taifa wa Botswana jana. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YAANZA KAZI CAF

## Yaiangushia Galaxy kitu kizito kichwani, Bocco, Lwanga wafanya yao mapema tu huku...

**Na Adam Fungamwango**

DAKIKA tano tu za kwanza za mchezo wa raundi ya kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika, jana ziliwatosha Mabingwa wa Tanzania, Simba kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy kwenye Uwanja wa Taifa wa Botswana.

Walikuwa ni Taddeo Lwanga na nahodha John Bocco walioingia kambani mara mbili kwa kufunga mabao yaliyotokana na kona, kutoka kila upande wa goli.

Kona iliyopigwa dakika ya pili ya mchezo na Mzambia Rally Bwalya, nusura iliingia yenyewe, lakini kipa wa timu hiyo, Ezekiel Morake aliupangua na kusababisha kizaazaa golini, kabla ya Lwanga kuusukumizia nyavuni mpira ambao alikuwa akigombea kuupiga na Bocco.

Dakika tatu baadaye, kona fupi iliyochezwa na Bernard Morrison akimpelekea Bwalya ambaye alimimina langoni, ukachezwa na beki wa Jwaneng Galaxy kabla ya kumkuta Bocco ambaye aliujaza kambani na kuacha kipa Morake akishangaa.

Baada ya mabao hayo ya haraka haraka, Simba ilionekana kutulia na kubadilisha mfumo, wachezaji wengi wakirudi nyuma na kumwacha Bocco mbele, ili kulinda ushindi ilionao mkononi.

Dakika ya 30 Mphoyamodimo Keiponye aliruka juu kushinda mabeki wote wa Simba na kupiga kichwa mpira uliotokana na faulo, lakini Aishi Manula alikaa imara langoni.

Resaobaka Thaninyane, nusura awapatie bao wenyeji, baada ya kuufuma mpira uliookolewa kizembe na Shomari Kapombe, lakini shuti lake kali lilitoka pembeni kidogo mwa lango la Simba.

Kwa muda mwingi wa dakika 45 za kipindi cha pili, Simba ilionekana kucheza nyuma ya mpira ikiwaacha Jwaneng Galaxy kumiliki, huku yenyewe ikishambulia kwa kushtukiza.

Ni kipindi ambacho mpira ulipoa zaidi kwani pamoja na wenyeji kuutawala mchezo, lakini hawakufanya shambulizi hatari la maana, huku mipango yao mingi ikitibuliwa na beki mpya wa Simba aliyesajiliwa msimu huu kutoka DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Henoc Inonga 'Varane', ambaye alikuwa kikwazo kikubwa kwa washambuliaji wa Jwaneng Galaxy.

Kwenye mechi hiyo, Kocha Msaidizi Thierry Hitimana, ndiye aliokuwa benchi, huku Kocha Mkuu Didier Gomes akiwa jukwaani kwani bado hajapata leseni yake inayotambuliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Wakati mechi ikikaribia kumalizika, Simba ilifanya mabadiliko, ikiwatoa Bwalya, Morrison na Sadio Kanoute, na kuwaingiza Erasto Nyoni, Duncan Nyoni na Meddie Kagere, ambao kwa kiasi fulani walisaidia kuisogeza timu hiyo mbele, lengo ikiwa si kushambulia kwa kutafuta bao, ila wakimiliki mpira na kupoteza muda zaidi, mpango ambao ulifanikiwa.

Kwa ushindi huo Simba imepiga hatua moja kutinga kwenye hatua ya makundi ya ligi hiyo, kwani imewapa mtihani wenyeji wao wa kushinda mabao 3-0 ili kuweza kupindua meza.

Mechi ya marudiano itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumapili ijayo.

# Mayele aionya KMC kwa Yanga

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA tegemeo kwa sasa kwenye timu ya Yanga, Mkongomani Fiston Mayele, ametamba kuwa atafanya kazi yake ya siku zote ya kukwamisha mpira wavuni kwenye mechi ya kesho dhidi ya KMC, mechi inayotarajiwa kupigwa katika Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma.

Tayari kikosi cha Yanga kimetua jana salama Songea mkoani Ruvuma, kwa ajili ya mechi hiyo ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC, ambayo imepeleka huko mechi yao.

Akizungumzia kwenye maandalizi ya mechi hiyo, Mayele ambaye amekuwa gumzo kwa sasa kutokana na kufunga bao pekee kwenye mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, Septemba 25, mwaka huu, Yanga ikishinda bao 1-0, lakini kwenye mechi ya kirafiki Jumapili iliyopita dhidi ya JKU ya Zanzibar pia wakipata ushindi kama huo, straika huyo amesema itakuwa mechi ngumu kwa sababu wapinzani wao wataingia kwa nia ya kuwazuia, lakini ana uhakika wataibuka na ushindi kwa sababu wamedhamiria msimu huu kila mechi kuondoka na pointi tatu.

"Tunakwenda kucheza na KMC, tunajua kuwa itakuwa mechi ngumu, sisi kwetu mechi zote tunataka pointi tatu. Najua Fiston atafanya kazi yake kama kawaida, atakuwa akishirikiana na wenzake, basi hakuna kitakachoshindikana, mechi zote tunahitaji ushindi," alisema mchezaji huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ingawa mpaka sasa hajafunga kwenye mechi yoyote ya Ligi Kuu.

Nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto, alisema maandalizi ya wiki moja yaliyokuwa yakifanyika kwenye mapumziko ya mechi zilizo kwenye Kalenda ya FIFA, yamewafanya wachezaji kupata muunganiko zaidi.

"Timu imejiandaa vizuri, mchezo dhidi ya KMC naamini utakuwa mzuri na mgumu, lakini nia yetu ni kupata ushindi kwa sababu kila mechi ni fainali. Tunachoshukuru ni kwamba mapumziko haya tumekaa pamoja na kuzoeana, hii inatupa nguvu ya kuona kuwa tutafanya vizuri," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >